MID WEEK JACKPOT!
TZS. 728,573,060
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Jumatatu Oktoba 2, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581451
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 2
**Walimu** watembea kilometa 7 kwenda shuleni kufundisha



UKURASA WA 4
**Mkakati** kuongeza fedha wanazotuma diaspora wazinduliwa

UKURASA WA 4
**TRA** yaonywa utaratibu kudai kodi kwa nguvu



# Moto waacha kilio Kariakoo

• **Maduka** 995 yateketea, hoja ya CAG ya mwaka 2018 haijafanyiwa kazi... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 8
**WASHTUSHWA MAZAO KIDUCHU MBEGU MPYA**
BAADHI ya wananchi wa Kata ya Ngimu, Halmashauri ya Wilaya ya Singida...

UKURASA WA 9
**ADAIWA 'KUOA' MAMA, WATOTO WAKE WAWILI**
MATUKIO ya ukatili wa kijinsia yanazidi kuitesa Kata ya Mwika Kaskazini...


UKURASA WA 19
**JESHI LA POLISI LAINGIA MAKUBALIANO MIKOPO MAALUM KWA ASKARI**
JESHI la Polisi limeingia Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Benki ya Exim...



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wakizima moto uliokuwa unateketeza majengo ya biashara katika eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## CHADEMA yaona dosari mitaala mipya ya elimu

UKURASA 3



## Jokate anena kuteuliwa Katibu Mkuu wa UWT

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA HII IMEENDA** UK.24 **KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao maalum cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kilichofanyika jijini Dar Es Salaam jana. **PICHA: CCM MAKAO MAKUU**

# Moto waacha kilio tena Kariakoo

**Na Jenifer Gilla**

MOTO mkubwa umeibuka katika eneo la Big Bon, Kariakoo jijini Dar es Salaam na kuteketeza maduka takribani 1,000 yakiwamo ya vifaa vya magari yaliyo chini ya Kampuni ya Kariakoo Auction Mart na kusababisha hasara ya mamilioni ya shilingi.

Kwa mujibu wa mashuhuda, moto huo ulianza jana saa 12.30 asubuhi katika maduka ya kampuni hiyo na kusambaa hadi kwenye majengo jirani. Uharibifu mkubwa wa mali umeshuhudiwa huku baadhi ya watu wakijeruhiwa.

Mmoja wa mashuhuda, Abdallah Salehe, alisema alisikia kelele za moto eneo la Big Bon na alipokwenda, alikuta baadhi ya vibanda vikiwaka moto.

Alisema walifanya jitihada za kuzima moto huo baada ya Jeshi la Zimamoto kufika eneo la tukio wakiwa hawana maji. Moto umeteketeza mali huku madirisha, matangi ya maji na nyaya za umeme za maghorofa ya jirani nazo zikiharibiwa.

Alisema mpaka magari ya zimamoto yenye maji yenye nguvu ya kukabili moto huo yanafika, sehemu kubwa ya mali zilishateketea.

"Tuliangalia nyumba za jirani zilizokuwa na vifaa hatarishi vya kuchochea moto, ghorofa la jirani hapo tulidhibiti moto usiingie kwa sababu kulikuwa na madumu ya mafuta, ilichangia kwa kiasi kikubwa moto usishike kasi, "alisema.

Mmoja wa wafanyabiashara wa vifaa vya magari, Salum Said, alisema amepata hasara kubwa kwa kuwa aliwekeza maduka matatu ya vifaa hivyo ambayo yote yameungua na kumwacha hana chochote kwa kuwa hakuwa na bima.

Alisema wakiwa na wenzake walifanya tathmini katika eneo hilo na kugundua kuwa kati ya vibanda vya biashara takribani 1,000, vilivyoko katika eneo hilo, vitano tu ndivyo havikufikiwa na moto huo.

"Soko kubwa la Kariakoo lilipoungua, tuliushauri uongozi wetu twende tukakate bima kama kampuni ili kujilinda, lakini hawakufanya chochote. Matokeo yake moto umetukuta na kutuacha maskini," alilalama Salum.

Mfanyabiashara Hamis Saudi alisema wanahisi moto huo ni hujuma kutokana na mgogoro wa muda mrefu uliopo baina ya wafanyabiashara wenye hisa na viongozi wao.

Mwandishi wa habari hizi aliona viongozi wa kampuni hiyo wakiingia kwenye kikao wakihidi kuzungumza na waandishi baada ya kumaliza kikao hicho, lakini walipotoka hawakukubali kuzungumza lolote.

Mmiliki wa Jengo la Benki ya Baroda, Ally Khalfan, alisema moto huo ulifika katika jengo lake na kuathiri madirisha, nyaya za umeme na tangi la maji katika ghorofa ya nane, huku baadhi ya wapangaji wake wakipata majeraha wakati wakijiokoa.

Mfanyabiashara wa chakula, Mariam Abdallah, alisema ajali hiyo imeathiri biashara yake kwa kuwa wafanyabiashara hao ndio waliokuwa wateja wake wakubwa. Alikuwa anauza si chini ya sahani 200 za chakula kwa siku.

Jackson Davis, aliyekuwa anatengeneza simu zilizoharibika, alisema tukio hilo limemwingiza katika deni kubwa kwa kuwa simu zote za wateja zimeungua. Vifaa vyake vya kutengenezea simu vyenye thamani ya Sh. milioni 1.4 pia vimeteketea.

Kaimu Kamanda wa Jeshi na Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Ilala, Mrakibu Mwandamizi Elisa Mugisha alisema alipata taarifa ya moto huo saa moja asubuhi na kutumia dakika mbili kufika eneo la tukio.

Alisema walifanikiwa kudhibiti moto huo kwa kiasi kikubwa. Chanzo chake hakijafahamika. Watafanya uchunguzi na kuchukua tahadhari ya matukio kama hayo.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila alisema moto huo umeleta hasara kwa wafanyabiashara na wenye majengo, lakini hakuna kifo kilichotokea katika tukio hilo.

Waziri Mkuu Kivuli wa Kamati ya ACT Wazalendo, Dorothy Semu, alisema tukio hilo ni mwendelezo wa matukio makubwa ya moto kwa miaka miwili mfululizo katika maeneo ya biashara. Mwaka jana Soko Kuu la Kimataifa la Kariakoo liliungua na kusababisha hasara kwa wafanyabiashara zaidi ya 1,800 na maduka zaidi ya 220 yaliteketea bila uokoaji.

Alipendekeza Bunge liunde kamati ya kufuatilia na kuchunguza matukio haya ya ajali za moto nchini kwa haraka kubaini vyanzo na mapendekezo ya kukabiliana nayo.

Kilichoshuhudiwa Kariakoo jana kinatoa taswira kutotekelezwa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2018 kuhusu usalama wa majengo ya umma nchini.

Katika ripoti yake ya mwaka 2016/17, CAG alibainisha majengo mengi ya umma si salama dhidi ya moto kutokana na utekelezaji duni wa hatua za usalama dhidi ya moto kwenye majengo hayo. Alitoa hoja serikali ifanyie kazi dosari hiyo.

# Walimu walia kutembea Km 7 kwenda kufundisha

**Na Marco Maduhu,** MISUNGWI

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Ihelele, wilayani Misungwi mkoani Mwanza, Evidence Muganyizi amesema walimu shuleni huko wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilometa saba kufika shuleni kutokana na kutokuwa na nyumba za walimu na hata za kupanga jirani na shule.

Alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa Mahafali ya Kwanza ya Darasa la Saba ya shule hiyo yenye walimu saba, ikiwa na nyumba moja tu ya walimu anayoitumia. Walimu wengine wanaishi mbali na shule, takriban Km saba.

Ni dosari aliyoitaja inasababisha kupungua morali ya kazi na ufanisi wa ufundishaji wao kutokana na kufika shuleni wakiwa wamechoka.

"Moja ya changamoto ambayo inatukabili kama walimu katika shule hii ni kuishi umbali mrefu na shule. Kijiji hiki cha Ihelele hakina nyumba za kupanga, hivyo kulazimika kwenda kutafuta nyumba za kuishi mbali na shule, hali inayowachosha walimu kabla hata hawajaanza ufundishaji," alisema.

Shule hiyo iliyojengwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama, Shinyanga (KASHWASA) ilianza kutoa huduma mwaka 2017 ikiwa na wanafunzi 94 (wasichana 54), lakini wamehitimu 71 (wasichana 42 na wavulana 29).

Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya KASHWASA, Dk. Edith Kwezi, alisema changamoto zinazoikabili shule hiyo zitafanyiwa kazi ukiwamo ukosefu wa umeme, maji na uhaba wa nyumba za walimu.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza serikali kuhakikisha kila mwalimu anakuwa na nyumba kwa ajili ya makazi yake binafsi na familia yake. Iwe karibu na eneo la kazi (shuleni).

# Jokate alonga kuteuliwa Katibu Mkuu wa UWT

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU Mkuu mpya wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Jokate Mwegelo, ameahidi kutoa ushirikiano wa kutosha na kufuata maelekezo ya mwenyekiti wake.

Jana Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), ilikutana katika kikao chake maalum jijini Dar es Salaam na kufanya uteuzi wa makatibu wakuu wa Jumuiya za Umoja wa Wanawake (UWT) na Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM).

Kamati Kuu (CC) ilimteua Mwegelo kushika nafasi hiyo na kabla ya uteuzi huo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga.

Nipashe ilizungumza na Jokate kwa njia ya simu na kueleza kuwa anaishukuru Kamati Kuu wa CCM chini ya Mwenyekiti wake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumwamini na kumteua kushika nafasi hiyo.

"Nitafuata maelekezo ya mwenyekiti na ninaahidi ushirikiano wa kutosha kwa viongozi wote wa chama na serikali," alisema Mwegelo.

Jokate amewahi pia kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani na baadaye kuteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Korogwe.

Jokate anakuwa Katibu Mkuu wa nane baada ya nafasi hiyo pia kushikiliwa na Phillis Nyimbi, ambaye aliichukua kutoka kwa Queen Mlozi.

Wengine walioshika nafasi hiyo ni Amina Makilagi, Hasna Mwilima, Halima Mamuya, Kate Kamba na Leya Lupembe.

Wakati huo huo, NEC imemteua Fakii Lulandala, kuwa Katibu Mkuu wa UVCCM, kabla ya uteuzi huo alikuwa ni Mkuu Wilaya ya Momba mkoani Songwe.

Kamati Kuu imemteua, Hamad Khamis Hamad, kuwa mgombea wa CCM wa nafasi ya uwakilishi katika Jimbo la Matembwe.

"Kamati imempongeza Rais Samia kutokana na ziara aliyoifanya katika mikoa ya Lindi, Mtwara ambapo ilikuwa na mafanikio makubwa. Katika ziara hiyo pamoja na mambo mengine Rais Samia alikagua utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2020-2025 kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi changamoto za wananchi."

Aidha, Kamati Kuu imempongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa namna anavyoiongoza serikali katika kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mwenyekiti wa UWT Taifa kwa sasa ni Mary Chatanda ambaye alichukua wadhifa huo kutoka kwa Daudencia Kabaka.

Jokate ambaye alianza kufahamika kwenye ulimbwende, alikuwa mshindi wa pili kwenye taji la Miss Tanzania mwaka 2006, ambalo Wema Sepetu alikuwa mshindi.

Julai 28, mwaka 2018, Hayati Rais John Magufuli alimteua Jokate kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, akitokea kwenye nafasi ya Kaimu Katibu wa Idara ya Uhamasishaji na Chipukizi wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM).

Juni 19, 2021, Rais Samia Suluhu Hassan, alimhamisha kutoka Kisarawe na kuwa Mkuu wa Wilaya ya Temeke nafasi aliyodumu nayo hadi Januari 25, mwaka huu, alipohamishiwa Korogwe.

## HABARI KITAIFA




Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki anayeshughulikia masuala ya Afrika Mashariki, Balozi Stephen Mbundi (wa pili kulia), akibonyeza kitufe kuzindua rasmi dirisha la huduma za kibenki kwa Watanzania waishio nchi za nje (diaspora) inayojulikana kama 'NMB Kwetu'. Katikati ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, Mkurugenzi wa Masuala ya Diaspora wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi James Bwana (kulia), Ofisa Mkuu Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi (kushoto) na Balozi wa Tanzania nchini Uingereza, Balozi Mbelwa Kairuki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibamba: NEC ianzishe mfumo kusajili kielektroniki

**Na Beatrice Shayo**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeshauriwa kuanzisha mapema mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya usajili wa wapigakura, ili kuwawezesha wananchi kupata haki ya kupiga kura.

Ushauri huo ulitolewa na mwalimu wa masuala ya demokrasia, diplomasia na haki za vijana ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Deus Kibamba, kwenye mdahalo wa 'Kijana Nahodha' ulioandaliwa na Tanzania Youth Coalition (TYC) ili kuwaandaa vijana kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa 2024 na uchaguzi mkuu 2025.

"Tumezungumza kuhusu umuhimu wa kurahisisha uandikishaji wa wapigakura wapya yaani vijana wanapokuwa kwenye umri wa kupiga kura lazima kuwe na mfumo wa kuandikisha ambao utakuwa ni rafiki," alisema Kibamba na kuongeza;

"Kwa sasa vijana wapo mbio kutafuta maisha halafu ukamwambie akajipange kwenye foleni vijana wengi huwa hawajitokezi tumependekeza kuwapo na mifumo miwili wa kwanza mfumo wa kujiandikisha mwenyewe kwa kuwa vijana wengi wana simu za kisasa wanaweza kuelekezwa na kufundishwa na NEC."

Alisema Tume kazi yake ni kuandaa 'app' ili vijana waweze kujiandikisha na uhakiki wa taarifa kama ni sahihi.

Kibamba alisema kwa ambao hawawezi kujisajili kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wameona wasisubiri NEC iwafuate kuwaandikisha wamependekeza kuanzishwa mfumo wa mawakala.

"Huu mfumo unafanana na mfumo wa mawakala wa kusajili laini za simu hivi leo kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma kuna mawakala wengi wa kusajili laini na mfumo huo unafanya kazi vizuri tulioupendekeza unafanana na huo utasaidia yule ambaye hana uwezo wa kujisajili mwenyewe anatembea kidogo na kwenda kwenye mwavuli na kujisajili halafu anasubiri uhakiki wa taarifa zake," alisema Kibamba.

Kadhalika, alisema mfumo wa uchaguzi ni wa kidunia serikali nyingi zimeuingiza kidijitali na Tanzania kuna BVR vifaa ambavyo vilinunuliwa kwa gharama kubwa kwa ajili ya Tume kuwaandikisha wapigakura.

"Vijana walichokipendekeza badala ya kusubiri sheria inayoeleza Tume iweze kuandikisha wapigakura wapya angalau mara mbili ndani ya miaka mitano, hata hili limekuwa ni gumu kufanyika kutokana na bajeti na kushindwa kuandikisha mara mbili kama sheria inavyowataka," alisema Kibamba.

Alisema wamependekeza mfumo wa kupiga kura ukiwekwa kidijitali maana yake uchaguzi unaweza kukamilika saa kumi jioni na saa mbili usiku matokeo yanakuwa tayari.

"Kuliko hivi sasa makaratasi mpaka yakahesabiwe moja baada ya jingine wakati dijitali inapigwa na kujihesabu yenyewe imeonekana hizi gharama ambazo serikali inazitumia kupitia NEC ambazo ni kubwa ziweze kuboreshwa mfumo wa kukusanya karatasi kwa mkono na ku 'print' uweze kupungua wapo ambao hawataweza kupiga kura kwa dijitali watahitajika kufika kwenye vituo, lakini watakuwa ni wale walioamua kufika kituoni," alisema Kibamba.

Kuhusu changamoto za kuingilia mifumo, alisema zipo dunia nzima na wamependekeza mfumo kuimarishwa mtu asiweze kuingilia.

Eneo jingine ni kuhusu vijana wengi kuminywa na vyama kwenye kugombea na kupendekeza badala ya kutumika kwenye kuhamasisha na kushangilia, umri wa kugombea uwe ni kuanzia miaka 18.

Akifafanua alisema sheria ya sasa inakataza mtu akiwa na umri wa miaka 18 hadi 20 haruhusiwi kugombea chochote hata uenyekiti wa serikali za mitaa.

Kibamba alisema kwa kuwa serikali inapelekea marekebisho ya sheria za uchaguzi bungeni basi umri wa kupiga kura uwe ndio umri wa kugombea isipokuwa kwa nafasi ya urais.

Aidha, alisema eneo jingine vijana wengi wanashindwa kushiriki masuala ya mchakato wa uchaguzi kutokana na fedha na kupendekeza maombi ya vyama vya siasa kwa maana ya ruzuku kuanzia sasa ianze kutolewa kwa vyama vyenye wabunge bungeni na madiwani.

Aidha, alisema vijana hao wamependekeza mfumo wa mgombea binafsi ukianza itasaidia ambao hawajateuliwa na vyama vyovyote kugombea na baadhi yao wakachaguliwa.

"Yupo mgombea binafsi aliwahi kukishinda chama kikubwa kinatwa TANU. Iliwahi kumsimamisha mgombea Mbulu ambaye alikuwa hakubaliki na wapiga kura alidondoshwa na mgombea binafsi mara chache mfumo huu huwa unasaidia pale inapotokea kuna uonevu umetokea," alisema Kibamba.

Mkurugenzi wa TYC, Lenin Kazoba, alisema mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Kimarekani (USAID) ni wa miaka minne umelenga kuwafikia vijana 45,000.

Mradi umeanza mwaka huu na unakusudia kuongeza uwezeshwaji, uzalishaji na ushirikishwaji wa vijana kwenye masuala ya kijamii.

Kazoba alisema mradi utahakikisha vijana wananufaika na kujikwamua kiuchumi, kuwawezesha kuwa viongozi katika jamii zao kwa kuwaunganisha na maeneo yenye maamuzi nyeti ya kimaendeleo yanafanyika.

# CHADEMA yaona dosari mitaala mipya ya elimu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeitaka serikali kuacha kinachokiita kujimilikisha mchakato wa kuandaa sera ya elimu na mitaala mipya ya elimu, bali iwashirikishe wadau wote kwa kuwa jambo hilo limebeba maslahi ya taifa.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali yanayoendelea nchini.

"Si sawa serikali ikajimilikisha mchakato wa upatikanaji sera na mitaala mipya ya elimu nchini. Mjadala wa elimu haupaswi kujadiliwa na kuridhiwa na serikali peke yake.

"Mapendekezo yaliyotolewa kuhusu mitaala na sera ya elimu hajajitosheleza katika kuvusha nchi yetu kwenda mbele," Mnyika alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema serikali inatakiwa kupata mapendekezo ya kuboresha mfumo wa elimu nchini toka katika makundi yote kwa kuwa watu wote watakwenda kunufaika na maboresho hayo bila kujali chama.

Mnyika alisema kwa namna ambavyo mchakato huo umendesha hadi ulipofikia sasa, CHADEMA hawajaridhishwa na mapendekezo yaliyotolewa ambayo wanaona yanahitaji kuboreshwa ili kupata mfumo wa elimu ulio bora na shindani kimataifa.

Pia alisema kuwa hivi sasa serikali inaandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 ambayo pia kwa kiasi kikubwa wao hawajashirikishwa.

"Haiwezekani chama kimoja kuandaa Dira ya Taifa ya hadi mwaka 2050 bila sisi kushirikishwa, dira ambayo ni ya miaka mingi ambayo kama sisi tukiingia madarakani tutatakiwa kuitekeleza, lakini leo hii hatushiriki katika kuiandaa.

"Haiwezekani! Hata kama hatupo serikalini, lazima kuwapo mlango wa sisi kushiriki katika kuandaa jambo hili," alisisitiza.

Alitaka serikali itoe kauli ya kuelekeza mchakato mzima wa uandishi wa Dira ya Taifa ufanywe kwa kushirikisha makundi mengine.


**KUPOTELEWA NA CHETI**



**AIKA FRANK MWANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0264-0001** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BABRO JOHANSSON SEKONDARI** mwaka 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/19336/2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 479 LA 2023**

**LAWI S. MHOJA MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

(1) JULITHA C. SHAYO
(2) JAMES W. SHIJA & ATHUMANI ABDI RAME T/A MFALME INVESTMENT
(3) NMB BANK P.L.C
(4) ADILI AUCTION MARTS LTD....MDAIWA/WADAIWA

**WITO KUITWA SHAURINI**

(1) JULITHA C. SHAYO
(2) JAMES W. SHIJA & ATHUMANI ABDI RAME T/A MFALME INVESTMENT
(3) NMB BANK P.L.C
(4) ADILI AUCTION MARTS LTD

**POPOTE ULIPO/ MLIPO**

LAWI S. MHOJA amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 17/10/2023 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mh J.W. SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 27 mwezi 09 ,2023

**ANATAFUTWA NA POLISI KWA TUHUMA ZA WIZI**
**MFA/RB/2466/2023**

**Ndug. Lazarius Philipo Mbilinyi** anatafutwa na polisi kwa tuhuma za wizi katika kampuni ya **EAST AFRICA ZHENYUAN GROUP CO LIMITED MAFINGA** iliyopo Iringa maeneo ya Mafinga, mtuhumiwa anatumia pasi ya kusafiria yenye namba **TAE 591910**



117622802

Yeyote atakayefanikisha kutoa taarifa za kukamatwa kwa mtuhumiwa huyu zawadi nono itatolewa

***Kwa mawasiliano piga simu namba 0742 282 782 au toa taarifa kituo chochote cha Polisi***

# Mkakati kuongeza fedha wanazotuma diaspora wazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeanzisha dirisha maalum la kuhudumia Watanzania wanaoishi nje ya nchi, huduma ambayo serikali imesema itasaidia kuongeza fedha ambazo diaspora wanatuma na kuwekeza nchini.

Suluhisho hilo linaloitwa 'NMB Kwetu' lilizinduliwa rasmi mwishoni wiki ili kutoa huduma za kifedha kwa diaspora kwa kuwapa nafasi ya kufungua akaunti na kufanya miamala kidijitali na kuwekeza nyumbani kupitia benki hiyo.

Mgeni rasmi katika uzinduzi huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Stephen Mbundi, aliyemwakilisha Waziri January Makamba, alisema mbali na huduma hiyo kurahisisha utumaji wa fedha, pia itaongeza fedha za kigeni wanazotuma wana diaspora nyumbani. "NMB Kwetu ni huduma muhimu inayoenda kusaidia juhudi za serikali za kuhakikisha Watanzania wote kokote waliko wanapata huduma za kifedha, wakiwamo wale wanaoishi ughaibuni," Balozi Mbundi alibainisha.

Aliongeza kuwa serikali inatambua na kuthamini mchango wa diaspora katika ujenzi wa taifa kupitia utaalamu wao na fedha wanazotuma nyumbani ambazo zilifikia dola za Marekani milioni 369.3 mwaka 2021.

Balozi Mbundi alisema kiasi hicho kimekuwa kinaongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia dola bilioni 1.1 sawa na Sh. trilioni 2.6 mwaka jana ambapo diaspora walitumia Sh. bilioni 4.4 kuwekeza katika ununuzi wa nyumba na viwanja nchini.

Aliongeza kuwa Watanzania hao pia ni washiriki wazuri katika soko la mitaji na hisa ambapo mwaka 2022 waliwekeza Sh. bilioni 2.3 kwenye Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji (UTT).

"Bila shaka diaspora wetu watachangamkia na hatifungani ya NMB Jamii Bond ambayo sasa hivi iko sokoni," Balozi Mbundi alibainisha huku akitambua mchango wa Benki ya NMB katika shughuli za maendeleo.

Alisema mbali na kuwa jambo la kihistoria, huduma ya NMB Kwetu pia imekuja wakati mwafaka na inatoa fursa kwa benki hiyo kunufaika na miamala ya kimataifa. Balozi Mbundi aliongeza kuwa kipengele cha bima ya maisha cha suluhisho hilo kitatua changamoto ya muda mrefu ya wana diaspora pindi walipokuwa wanakabiliwa na madhila ya vifo au ulemavu wa kudumu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema mbali na fao la kifo na ulemavu, bima hiyo pia inagharamia usafirishaji maiti huku akitaja sifa kubwa ya kwanza ya NMB Kwetu kuwa ni kutengeneza mfumo wa kidijitali wa ukusanyaji nyaraka zinazohitajika kwa ajili ya kufungua akaunti.

"Suluhisho la pili kupitia NMB Kwetu ni Bima ya Maisha. Wana diaspora wote watakaofungua akaunti zao Benki ya NMB moja kwa moja watakuwa wameingia bima ya maisha yenye thamani ya hadi Sh. milioni 29. Bima hii ya maisha inatolewa kwa ushirikiano na Kampuni ya Bima ya Sanlam Life," alisema.

Alibainisha kuwa akaunti zote za NMB Kwetu hazitakuwa na makato ya kila mwezi kama akaunti nyingine. Utumaji fedha utaongezwa ufanisi na huduma ya Worldwide Pesa.

NMB ilianzisha huduma hiyo inayowezesha wana diaspora kutuma fedha nyumbani kwa ndugu, jamaa na marafiki kutoka nchi zaidi ya 100 duniani mwaka jana kwa kushirikiana na kampuni za Thunes na Terrapay. Pamoja na kutotangazwa, Zaipuna alisema mpaka sasa Worldwide Pesa tayari imefanikisha zaidi ya miamala 35,000 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 52.

# TRA yaonywa kudai kodi kwa nguvu

**Na Restuta James**



NAIBU Waziri wa Fedha, Hamad Chande (pichani), ameiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kutumia mbinu za kirafiki kukusanya kodi ili wafanyabiashara wengi zaidi waweze kulipa kodi kwa hiari.

Vilevile, amemwagiza Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata kuwatambua na kuwapa motisha wafanyabiashara wanaolipa kodi kwa wakati kila mwaka.

Chande aliagiza hayo mwishoni mwa wiki alipofunga Wiki ya EFD inayotumika kutoa elimu ya kodi kwa wafanyabiashara na wananchi katika Soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Alisema Watanzania ndio wenye jukumu la kujenga nchi yao kupitia mapato ya serikali yanayokusanywa na TRA ambayo yanaelekezwa katika huduma muhimu za kijamii kama ujenzi wa miundombinu ya elimu, barabara na afya.

"Kila mtu anayestahili kulipa kodi alipe kwa hiari na kwa wakati. Miaka ya nyuma mtumishi wa TRA alikuwa anaonekana adui mkubwa kwa sababu walikuwa wanatumia mbinu ambazo sio rafiki, lakini leo tunaona mnatumia mbinu rafiki. Endeleeni kujenga uhusiano mzuri ili watu wafurahie kulipa kodi," alisema.

Chande aliongeza kuwa mbinu hiyo itawawezesha wafanyabiashara kulipa kodi kwa wakati ili serikali itekeleze azma yake ya kuwapelekea wananchi maendeleo.

Pia aliwataka watumishi wa mamlaka hiyo kuzingatia weledi na uwajibikaji katika utendaji wao kwa kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Kuhusu motisha, alisema maadhimisho ya Wiki ya EFD yanapaswa kutambua wafanyabiashara wa ngazi mbalimbali kuanzia wadogo, wa kati na wakubwa wanaowasilisha kodi kwa wakati kwa kuwapa vyeti.

Kamishna Mkuu wa TRA, Kidata alisema matumizi sahihi ya EFD yataiwezesha mamlaka hiyo kufanya makadirio halali kwa wafanyabiashara na kuondoa malalamiko ya makadirio makubwa. "Ninawaomba Watanzania tuwe wazalendo kwa kulipa kodi, TRA inataka ikusanye kodi halali na wala sio kubambika, tukiwajibika hutogombana na maofisa wa TRA," alisema.

Wasambazaji kutoka kampuni ya Radix, Mojatax, Softnet, Zalongwa na Advatech, walisema hivi sasa mashine za EFD zimeboreshwa na hivyo kumwezesha mfanyabiashara kutoa risiti ngumu na laini kulingana na mahitaji ya mteja.

SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

## INVITATION FOR TENDERS

1. Tanga Cement Public Limited Company is hereby soliciting bids from interested eligible companies and individuals to supply Personal Protective Equipment (PPE) commencing 1 December 2023.

2. Interested eligible bidders may obtain a complete set of bidding documents from the office of the Procurement Manager located at Tanga Cement premises in Tanga between 08H00 and 14H00 Mondays to Fridays (excluding public holidays).

3. Sealed bids must be deposited in the Tender Box located at Tanga Cement visitors' gate in Tanga by **12H00** on the **16 October 2023.**

4. Sealed tenders and modifications thereof must be deposited in the Tender Box located at the visitors' gate by 12H00 on the closing date indicated above. All tenders submitted must remain valid for t**he period specified in the tender documents** from the closing date indicated above. All tenders must be sealed, marked with the **relevant correct tender title**, and addressed to:

**The Managing Director**
**Tanga Cement Public Limited Company**
**P.O. Box 5053**
**Tanga**
**Tanzania**

5. This invitation to bids does not in any way constitute an offer to a contract or bind the Company in any way.

6. The bidding documents will be purchased by interested bidders and collected upon payment of non-refundable fee **Tanzanian Shilling (TZS) 100,000.00 (one hundred thousand)** through either of the below bank details.

| Bank Name | Account number | Account Name |
|---|---|---|
| CRDB Bank | 0150385602300 | Tanga Cement PLC |
| NMB Bank | 41710039344 | Tanga Cement PLC |

7. All bidders must have the approved relevant level of **"local content"** as required by the Mining Commission

8. Any explanation desired by prospective bidders on the meaning or interpretation of this solicitation must be requested in writing to **Mr Sieddy Gimbi** at *sieddy.gimbi@simbacement.co.tz*

9. Schedule of tenders

| S/N | Tender number | Tender Tittle |
|---|---|---|
| 1 | TCPLC-10-2023 | Supply of Personal Protective Equipment (PPE) |

# Kliniki za ardhi zatajwa mkombozi kwa wananchi

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

KUWAPO kliniki za ardhi katika Halmashauri ya Chalinze kumetajwa kuwa mkombozi wa wananchi waliokuwa wanatembea umbali mrefu kwenda Bagamoyo na Kibaha kwa ajili ya kesi za migogoro ya ardhi ambayo sasa ufumbuzi wake utafanyika kupitia kliniki hizo.

Ofisa Ardhi wa Halmashauri hiyo, Deo Msilu, aliiambia Nipashe mwishoni mwa wiki kuwa katika kliniki hiyo ambayo itakuwa inazunguka kwenye kata za Bwilingu, Vigwaza na Msata, wananchi wa kata hizo na za karibu watafika kupatiwa huduma za kisheria kulingana na kero zao.

Msilu alibainisha hayo muda mfupi baada ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash kuzindua kliniki hiyo mjini Chalinze kwa ajili ya halmashauri hiyo.

Kliniki hiyo ya Halmashauri ya Chalinze imezinduliwa ikiwa ni siku chache baada ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa kuizindua katika ngazi ya wilaya.

Msilu alibainisha kuwa katika kliniki hiyo wananchi wenye malalamiko na migogoro ya ardhi watapata huduma kutoka kwa wanasheria na mawakili bila malipo.

Kwa mujibu wa Msilu, migogoro ya ardhi ambayo imeshamiri katika halmashauri hiyo ni ya wakulima na wafugaji, mipaka kati ya kijiji kimoja na kingine na uvamizi wa maeneo ya serikali, hifadhi na mashamba yaliyotelekezwa.

"Kata zinazoongoza kwa migogoro ni Ubena, Mbwewe na Kiwangwa, maeneo yote hayo tumeshapita kutoa elimu na tunaendelea kufanya hivyo ili wajue sheria na kuziheshimu kwa kuwa kwa kufanya hivyo itapunguza mwingiliano kwenye matumizi ya ardhi," alifafanua.

Salma Mrisho, mkazi wa Chalinze, alipongeza uamuzi wa serikali kuanzisha kliniki hizo ambazo zitawapa fursa ya kusikilizwa malalamiko yao sambamba na kupunguziwa gharama za kutembea umbali mrefu kwenda kupata huduma hiyo.

Katika siku ya kwanza ya uzinduzi wa kliniki hiyo ya Halmashauri ya Chalinze, zaidi ya wananchi 30 walijitokeza kupata huduma.

Sudi Saidi, Mkazi wa Pera, alisema hatua hiyo inakwenda kupunguza kero za migogoro ya ardhi ambazo zimekuwa zikikwamisha maendeleo kutokana na wananchi kutumia muda mwingi kwenda mahakamani na vyombo vingine vya sheria.

Katika Mkoa wa Pwani, eneo linaloongoza kwa migogoro ya ardhi ni Mapinga ambako Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge amekuwa anazuru mara kwa mara, akiambatana na wataalamu wa kitengo cha sheria na ardhi kutatua migogoro hiyo.

Katika kushughulikia eneo hilo, Kunenge ameshaonya kuwa yeyote anayehusika kushiriki uvamizi wa maeneo ambayo yana umiliki, hatua za kisheria zitachukuliwa kukomesha tabia hiyo ambayo imekuwa ikifanywa kwa maeneo ambayo hayajaendelezwa na yale ya serikali.

TOLEO MAALUM

# Mpango mpya wa lishe bora kutoka Yara Tanzania kukuza tija sekta ya mifugo, uvuvi




Mkuu wa Mkoa wa Iringa Halima Dendego na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Mbolea ya Yara Winstone Odhiambo wakizindua rasmi bidhaa za lishe ya mifugo iliyo tambulishwa na kampuni hiyo katika hafla iliyofanyika mjini Iringa juma lililopita



## Aina mpya ya lishe ya mifugo kutoka Yara Tanzania

1. **Kynofos 21** Ni bora kwa broilers na kuku wa mayai, samaki, nguruwe na wanyama kama paka;

Faida
- Inaongeza kiwango cha ukuaji kwa wanyama.
- Inaongeza uzalishaji na mayai.
- Inaimarisha ubora wa ganda la yai.
- Inaboresha utotoleshaji wa vifaranga.

2. **Maziwa Pro** ni mahususi kwa ajili ya ng'ombe wa maziwa. Ina Kiwango kikubwa cha chembechembe za madini ya Phosphorus. Pia imerutubishwa na sukariguru na asilimia 15 ya protini.

**Faida**
- Inaongeza uzalishaji na ubora wa maziwa.
- Inachochea joto la kupandwa na kushika mimba.
- Kuzuia ulaji ovyo wa mifuko ya plastiki na vitu vya jamii ya miti/mbao.
- Inaongeza kinga ya mwili na kupunguza changamoto za magonjwa.

3. **Kalori 3000** ni bidhaa ya unga mkavu wa kunyunyiziwa sukariguru (Molasses)

**Faida**
- Kuongeza ladha na ulaji wa chakula.
- Kuboresha umeng'enywaji wa chakula kwa wanyama wanaocheua.
- Inaimarisha kuchachushwa kwa majani yaliyovundikwa [Silages]
- Inahakikisha usahihi wa ubora wa madini kwenye jiwe la kulamba.
- Huongeza uzalishaji kwa ng'ombe wa maziwa.
- Inachochea unenepaji wa haraka kwa mifugo wa nyama.

4. **Feed Grade** Urea ni chakula ambacho ni chanzo rahisi cha protini kwa ajili ya wanyama wanaocheua

**Faida**
- Huboresha ukuaji wa Wanyama.
- Huboresha umeng'enywaji wa chakula, nyasi kavu.
- Huongeza uzalishaji wa maziwa.
- Inachochea unenepaji wa haraka kwa mifugo wa nyama.

5. **Kimtrafos 12 Grande** ni chakula cha Phosphate yenye wingi wa madini madogomadogo mahususi kulisha ng'ombe (wa nyama na maziwa), kondoo na mbuzi.

**Faida**
- Ina madini yote madogomadogo katika uwiano ulio sahihi kwa phosphorus.
- Haina vumbi ili kurahisiha maandalizi na uchanganyaji
- Ina sukariguru (molasses) ya unga ili kuongeza ladha na ulaji wa phosphorus.
- Inaongeza kiwango cha uzalishaji maziwa.

6. **Phospro 17** Ni Phosphate ya chumvi na protini kwa ajili ya chakula cha mifugo. Nzuri kwa ng'ombe, mbuzi, kondoo na wanyama pori wanaofugwa wakati wa kiangazi au wanaolishwa majani makavu.

**Faida:**
- Ina zaidi ya madini 8 na kuboreshwa na sukariguru ya unga yenye 17% protini.
- Inaboresha umeng'enywaji chakula na hamu ya kula wakati wa kiangazi.
- Inaimarisha ukuaji na uzazi wa mifugo.
- Stahimilivu kwa hali ya hewa na inaweza kuwekwa nje kwenye mvua.

7. **Feed Grade Sulphur** ni chakula cha mifugo ambacho kina Sulphur inayosaidia wanyama wanaocheua kuchakata amino asidi, methionine na lysine.

**Faida**
- Huongeza uzalishaji maziwa kwa ng'ombe wa maziwa.
- Inaongeza kiwango cha uzazi na ndama wenye afya
- Inaboresha ngozi na mwonekano angavu wa mnyama.
- Kupunguza hatari ya magonjwa.
- Huongeza ufanisi wa matumizi ya urea ya chakula cha mifugo.

**Na mwandishi wetu**

Kutambulishwa katika soko la Tanzania kwa aina mpya ya bidhaa bora za lishe ya mifugo kutoka Yara bila shaka kutakuwa ni hatua muhimu katika maendeleo ya sekta ya mifugo na uvuvi nchini. Uzinduzi wa bidhaa saba za kiwango cha juu na himilivu katika mazingira kwa mifugo, kuku na ufugaji wa samaki uliofanywa na Yara Tanzania Septemba 19, 2023, umeonyesha kwa vitendo dhamira ya kampuni hiyo katika kuchangia usalama wa chakula nchini, kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kanuni bora za kilimo zenyetija.

Ujio huo wa aina mbalimbali za vyakula vya mifugo kutoka Yara utaleta maendeleo chanya kwa Tanzania, na imekuja mara baada ya Tanzania kuandaa Kongamano la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) lililofanyika mapema mwezi Septemba kwa mafanikio makubwa.

AGRF pia ni jukwaa kuu la dunia la kilimo na mifumo ya chakula barani Afrika.

Mkutano huo uliwaleta pamoja zaidi ya wadau 5000 kuchukua hatua za kiutendaji na kuchochea mawazo yanayolenga kuendeleza mifumo ya chakula Afrika.

Yara International ni mshirika mkuu wa AGRF na inafanya kazi katika nchi zaidi ya 160, ikiwa ni pamoja na Afrika, ikifanya kazi na mamilioni ya wakulima kushughulikia changamoto za uzalishaji na ustawi wao.

"Kwa kuingia katika soko la lishe ya mifugo, Yara Tanzania inaiishi dhamira ya AGRF na pia kuendele- za azma yake kimataifa ya "Kukuza kilimo endelevu, ustawi shirikishi na kuhimili mabadiliko ya tabianchi," anasema Winstone Odhiambo, Mkurugenzi Mkuu wa Yara Tanzania na Rwanda.

Mpango wa Yara ni kuwawezesha zaidi ya wakulima milioni 50 ifikapo 2030 duniani kote. Tanzania na Rwanda ni nchi za tatu na nne barani Afrika mtawalia kuanzisha suluhisho ya lishe ya mifugo baada ya Afrika Kusini na Kenya.

Yara ni watengenezaji wa kimataifa wa vyakula bora vya mifugo kwa kiwango cha ubora wa kimataifa katika viwanda vyake vya uzalishaji vilivyopo Kokkola (Finland) na Durban (Afrika Kusini) ambavyo husambazwa katika nchi 70 duniani.

"Bidhaa zetu mpya za lishe ya mifugo zitaleta athari chanya katika ufugaji kwa kuboresha afya ya mifugo, kuongeza uzalishaji wa nyama, maziwa, mayai na samaki, na pia kupunguza athari za mazingira zinazotokana na ufugaji.

"Dhamira yetu ni kuwawezesha wakulima kustawi huku tukichangia maendeleo endelevu," anasema bwana Odhiambo, na kuongeza kuwa wasindikaji wa vyakula vya mifugo pia watafaidika na mchanganyiko wa lishe ya mifugo ya Yara ili kuboresha uborawa bidhaa zao.

"Hii kwetu sio ajenda ya ushindani ila tunatoa fursa ya kushirikiana kuleta mageuzi makubwa katika soko la chakula cha mifugo kwa faida ya wakulima, wauza bidhaa na uchumi kwa ujumla." Wafugaji na wazalishaji wa vyakula vya mifugo wameikaribisha Yara katika soko la chakula cha mifugo ili kukabiliana na uhaba na ubora duni wa bidhaa hizo ambao umekuwa changamoto kubwa.

Bidhaa chache na duni za lishe za mifugo zimerudisha nyuma tija na kuvuruga mnyororo mzima wa thamani.

> Tunafuraha kuwa Yara Tanzania inaleta bidhaa za vyakula vya mifugo vyenye virutubisho vingi. Tuko tayari kutoa maarifa ya bidhaa hizi ili kuwasaidia wafugaji wadogo kuongeza tija."
>
> FAUD ABRI | Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya ASAS Dairies ya Iringa.



Changamoto zinazozidi kuongezeka za janga la Uviko-19 na kupanda kwa bei ya nafaka wakati wa vita nchini Urusi na Ukraine kulizidisha hali hiyo, huku wakulima walioelemewa na mizigo wakilazimika kuachana na vyakula vinavyozalishwa viwandani na badala yake kuelekeza rasilimali nyingi katika kuzalisha vyakula wenyewe. "Tunafuraha kuwa Yara Tanzania inaleta bidhaa za vyakula vya mifugo vyenye virutubisho vingi.

Tuko tayari kushirikiana na Yara kutoa maarifa ili kuwasaidia wafugaji wadogo kuongeza tija," alisema Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya ASAS Dairies ambayo ni wazalishaji na wasindikaji wakubwa wa maziwa nchini, bwana Fuad Abri alipokuwa mwenyeji wa timu ya viongozi wa Yara Tanzania walipotembelea ofisi na mashamba ya kampuni hiyo mkoani Iringa.

Abri alisema ni wakati wa kuunga mkono juhudi kama wafanyabiashara wenye lengo moja la kubadilisha fikra za wakulima ili wafuge kisasa, kwa ubora na uendelevu.

Licha ya kuwa nchi ya tatu barani Afrika kwa idadi kubwa ya mifugo, Tanzania ina upungufu wa uzalishaji wa maziwa lita bilioni 9 kila mwaka, ikitumia zaidi ya Sh 30 bilioni kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje ili kufidia pengo hilo.

Wafugaji wadogo mkoani Iringa, Baraka Kibugu, Majoeno Ziangi na Simeon Kikoti walionyesha matumaini kuwa bidhaa hizo mpya za Yara zitaboresha uwekezaji wao.

"Tuna uhakika kwa sababu Yara ina chapa bora za mbolea na imejijengea sifa ya kushirikiana na wakulima na wasambazaji," alibainisha Kikoti.

Kwa upande wake Ziangi alisema; "Kupatikana kwa lishe bora kutabadilisha uwekezaji wangu.

Tunatoa wito kwa Yara kuzingatia vifungatio vidogo vya chakula cha mifugo vya bei nafuu kwa wafugaji wengi wadogo.

Tunafurahi kuwa bidhaa hizo zinakuja na viwango vya ubora vilivyothibitishwa kimataifa." Bwana Odhiambo alisema Yara Tanzania itahakikisha kuwepo kwa vifungashio ambavyo wafugaji wakawaida watavimudu kupitia mawakala wao waliopo maeneo mbalimbali nchini.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi miundombinu AFCON 2027 yaende sambamba na timu

**KWA** mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa michuano ya Mataifa ya Afrika 1957 (AFCON), mwaka 2027 itafanyika Ukanda wa Afrika Mashariki (Cecafa), ikiandaliwa kwa ushirikiano wa nchi tatu, Tanzania, Kenya na Uganda.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya mataifa hayo ya Cecafa ambayo yaliomba kuandaa kwa pamoja, kushinda maombi yao ya kuandaa michuano hiyo kwa kupata kura nyingi zaidi wiki iliyopita jijini Cairo, Misri dhidi ya Algeria, Misri na Botswana, ambazo nazo ziliomba.

Hivyo, kinachotakiwa kwa sasa ni maandalizi ya miundombinu ya viwanja, barabara nzuri pia hoteli za kisasa, vifaa tiba katika hospitali zaidi katika miji ama majiji fainali hizo zitakapofanyika.

Tunatambua zipo faida nyingi zitakazopatikana kutokana na nchi husika kuandaa michuano hiyo baadhi ni pamoja kutangaza utalii wa nchi, fedha nyingi za kigeni kupatika, biashara nyingi kufanyika na nyingine nyingi.

Hivyo, ni wakati sasa wa kufanya maandalizi makubwa ili tusinyang'anywe fursa hii kwani pamoja na kushindi ombi hilo kama tukishindwa kukamilisha maandalizi yanayotakiwa moja kwa moja tutany'ang'anywa na kupelekwa kwa walio tayari jambo ambalo hatutamani kuona likitokea.

Katika hilo, tunaamini serikali itafanya kila liwezekano kukamilisha maandalizi ya miundombinu hususan viwanja, barabara, uboreshwaji wa viwanja vya ndege, hospitali pamoja na vifaa tiba na mambo mengine wanayopaswa kushughulikia huku wakihakikisha amani inaendelea kutamalaki nchini kwani hicho nacho ni kipengele muhimu kuliko vyote.

Lakini pia ni wakati muafaka kwa wadau wa soka, wafanyabiashara kuwekeza katika ujenzi wa hoteli kubwa za kisasa pamoja na vivutio vingine ili timu zitakazopangwa kucheza Tanzania kupaona ni sehemu sahihi ya kupatembelea mara kwa mara kwa utalii.

Wakati hayo yote yakifanyika pia ni muda mwafaka kwa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwa kushirikiana serikali, kumwezesha Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Adel Amrouche, kuiandaa vema kwa fainali hizo ili muda utakapowadia iende kushindana na si kuishia kushiriki tu.

Ingawa inaonekana mwaka 2027 ni mbali, lakini kwa maandalizi ya timu ya kwenda kushindana na si kushiriki tu, miaka mitatu ni michache sana, hivyo Stars inapazwa kuandaliwa vilivyo kwa progamu mbalimbali kuanzia sasa.


Hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wachezaji wanaokitumikia kikosi cha Taifa Stars kwa sasa, mwaka 2027 baadhi umri na viwango huenda vikawa vimewatupa mkono, hivyo kutoweza kutoa upinzani ipasavyo.

Hivyo, kuna haja ya kocha Amrouche kuwezeshwa kumulika kila kona ndani na nje ya nchi kwenye wachezaji wa Tanzania wenye uwezo kuitwa kila mechi za kirafiki ama za kimashindano Taifa Stars inazocheza ili kuwafanya kuwa kundi moja lenye lengo moja la kuiwakilisha nchi ipasavyo.

Kwa upande wa serikali hata kama suala la uraia pacha ambalo limekuwa likipigiwa kelele kwa muda mrefu na wadau wa soka, haitaki kuliridhia, ione haja sasa ya kuutoa angalau kwa wanamichezo wanaoweza kuitangaza vema nchi yetu kimataifa na kuiletea medali.

Tunachotaka kukiona katika fainali hizo za AFCON 2027, si tu Tanzania kuandaa na kushiriki, bali pia kuweka rekodi kwa mara ya kwanza zikichezwa nchini inafika angalau nusu fainali, jambo ambalo dhamira ya dhati ikiwapo kuanza sasa inawezekana kabisa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Yanga sasa itafute mbadala wa Mayele hatua ya makundi Afrika

Na Adam Fungamwango

**ILIKUWA** ndiyo lengo namba moja kwa Klabu ya Yanga kutinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa barani Afrika msimu huu na kweli imefanikiwa kufanya hivyo.

Baada ya kufanikiwa kufika fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu uliopita, viongozi wa klabu hiyo walibainisha kuwa msimu huu wanachotaka ni kutinga hatua ya makundi Afrika kwani ilikuwa ni ndoto yao kwa takriban miaka 25 sasa.

Juzi imefanikiwa kuhitimisha ndoto hizo kwa kuitoa timu ya Al Merrikh kwa jumla ya mabao 3-0, ikishinda bao 1-0, na kabla ya hapo ilikuwa imeshinda mabao 2-0 nchini Rwanda.

Yanga imeitoa timu ambayo ni zoefu kuingia hatua ya makundi, lakini msimu huu inaonekana kukutana na mfupa mgumu, ikichagizwa pia na hali mbaya ya kisiasa nchini Sudan.

Ndiyo maana ilikwenda kuchezea mechi zake nchini Rwanda badala ya Sudan, lakini pia ikiwa na wachezaji wachache sana wa kigeni tofauti na mwanzo kwa sababu baadhi yao hasa wale mastaa waliondoka kutokana na nchi kutokuwa kwenye hali ya usalama.

Kabla ya hapo, Al Merrikh jambo la kuingia makundi ilikuwa si stori kwani ilikuwa ikifanya hivyo kila msimu, ingawa tatizo lao kubwa haikuwa inafanya vema ikiwa huko na ndiyo mara kwa mara wanakuwa vibonde wa kundi inalopangiwa.

> **Kabla ya hapo, Al Merrikh jambo la kuingia makundi ilikuwa si stori kwani ilikuwa ikifanya hivyo kila msimu, ingawa tatizo lao kubwa haikuwa inafanya vema ikiwa huko na ndiyo mara kwa mara wanakuwa vibonde wa kundi inalopangiwa.**

Naipongeza Yanga kwa kuweza kufanikisha ndoto hiyo na isingekuwa bora timu iliyofika hatua ya fainali Kombe la Shirikisho, msimu huu kushindwa kutinga japo makundi.

Niliwasikia baadhi ya viongozi wa timu hiyo wakisema lengo namba moja ni kutinga makundi na baada ya hapo watakaa na kuangalia lengo namba mbili timu ifike hatua gani. Lakini hiyo itategemea na jinsi viongozi watakavyojipanga kwa mambo mbalimbali ya kimkakati, kifedha na kiufundi pia.

Wanaweza wakatuambia kuwa lengo lao ni kufika hatua ya robo fainali au nusu, hii itategemea na wao wenyewe watakavyoona inafaa.

Ukiangalia kikosi cha Yanga tangu msimu uliopita kiko vizuri na kimetengenezwa kiushindani haswa ndiyo maana kikafanikiwa kutinga hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho.

Hata hivyo, kwa maoni yangu kuelekea kwenye hatua hiyo kinafaa kuongezewa nguvu na hasa kwenye safu ya ushambuliaji. Ni ukweli usiopingika tangu alipondoka Fiston Mayele kwenda kujiunga na Pyramids ya Misri haijawa na straika hasa ambaye unaweza kusema muda wowote uwanjani atakupa bao.

Badala yake msimu huu imepata bahati ya kuwa na viungo washambuaji ambao ni wafungaji kama Pacome Zouzoua na Maxi Nzengeli, lakini Stephane Aziz Ki msimu huu amekuwa wa moto kwenye kupachika mabao.

Inakokwenda ni kugumu kwani huku ilikoingia kuna timu ambazo utafikiri ndiyo maskani kwao. Timu hizo ni Al Ahly ya Misri, Wydad Casablanca ya Morocco, Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Esperance ya Tunisia na zingine.

Hizi huwa ni kama zimejiwekea ufalme wao tofauti na Kombe la Shirikisho. Zinacheza kwenye makundi, robo, nusu, fainali na kutwaa ubingwa na ni ngumu mno kuziondoa, hivyo kama una mastaika wa kawaida tu timu inakuwa kwenye wakati mgumu.

Bahati nzuri baada ya kumalizika kwa hatua hizi, kabla ya kuanza kwa makundi kuna kipindi cha usajili. Nafikiri ni wakati wa Yanga kumsaka straika mmoja tu mwenye uwezo mkubwa wa kutumbukiza mpira wavuni kusaidiana na Clement Mzize na Kennedy Musonda kwa ajili ya kupachika mabao na kusumbua mabeki wa aina ya klabu za Al Ahly pale mbele.

# DC, mbunge wakemea uvamizi katika mgodi

**Na Faustine Feliciane, aliyekuwa**
TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mtenjele na Mbunge wa jimbo hilo, Mwita Waitara, wamekemea vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wananchi vya kuvamia maeneo ya mgodi wa kuchimba dhahabu wa Barrick North Mara.

Viongozi hao wameagiza viongozi wa vijiji vinavyozunguka mgodi huo kutoa elimu na kuwaelimisha wananchi wao kuacha vitendo hivyo vinavyoleta uvunjifu wa amani na wakati mwingine vifo.

Katika mkutano wa pamoja wa viongozi wa Mkoa wa Mara, viongozi wa Barrick na wadau wengine wa maendeleo, Kanali Mtenjele alisema serikali haikubaliani na uvamizi unaofanywa na baadhi ya wananchi na kuwataka kutafuta shughuli nyingine za kuwaingizia kipato.

"Haya yanayotokea katika wilaya yetu kwa kweli hatukubaliani nayo. Jeshi la Polisi litaendelea kufanya kazi yake, lakini wananchi ambao wamekuwa wanafanya vitendo hivi ninawaomba waache.

"Zipo shughuli nyingi za kiuchumi, vijana wengi ndio wanaofanya vitendo hivi. Niwaombe waache kwa sababu mkono wa sheria utafanya kazi yake," alionya Kanali Mtenjele.

Aliuomba uongozi wa Mgodi wa Barrick North Mara kuendelea kubuni miradi ya maendeleo kwa wananchi wanaozunguka mgodi huo ili kuondoa kero hiyo ya vijana kuvamia maeneo ya migodi kwa lengo la kusaka mawe ya dhahabu.

"Ipo miradi ambayo inaendelea kutekelezwa, lakini niwaombe wenzetu wa Barrick waendelee kubuni miradi ya kiuchumi kwa ajii ya vijana wa maeneo yanayozunguka mgodi, hii itasaidia kuwapa nafasi ya kujiongezea kipato," alisema.

Mbunge Waitara alisema vijana wengi wanaovamia migodi ni wale waliokuwa wanafanya shughuli za uchimbaji kabla ya ujio wa mgodi huo, hivyo ni vyema wakapewa elimu na kutafutiwa miradi ya kufanya.

"Hatuna tatizo na Mgodi wa North Mara, wamekuwa wadau wetu wakubwa katika maendeleo kwenye wilaya yetu. Hawa vijana wanaofanya vitendo vya kuvamia maeneo ya mgodi waache kufanya hivyo, mwisho wake si mzuri.

"Ipo miradi ambayo wenzetu hawa wa mgodi wameianzisha kwa ajili ya kuwapatia kipato wananchi. Ninawasihi wananchi kushiriki katika miradi hii," alisema Waitara.

Mbunge huyo alisema anaamini siyo vijana wa maeneo ya jirani na mgodi wanaofanya vitendo hivyo, bali pia wapo vijana kutoka mbali na maeneo hayo.

Rais na Mkurugenzi wa Kampuni ya Barrick wanaomiliki Mgodi wa North Mara na Bulyanhulu mkoani Shinyanga, Dk. Mark Bristow, alisema kampuni hiyo itaendelea kushirikiana na serikali katika kutatua changamoto mbalimbali.

Alisema Wilaya ya Tarume ina nafasi kubwa ya kuzuia wavamizi wa mgodi kwa kuwa wanawafahamu wanaovamia.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (wa pili kulia), akikabidhiwa zawadi na Balozi wa Netherlands hapa nchini, Wiebe de Boer (wa pili kushoto), katika warsha ya siku moja kuhusu umuhimu wa kuongeza ushindani kwenye sekta ya vyakula vya mifugo vyenye protini iliyoandaliwa na ubalozi huo kwa kushirikiana na Mpango wa Kukuza Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo, Geoffrey Kirenga na Mkurugenzi wa Ufugaji wa Samaki kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Nazaeli Madalla (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa: Risiti EFD zitokane na mashine zilizothibitishwa

**Na Mwandishi Wetu,**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wakuu wa wilaya kupitia kamati za mapato za wilaya wakutane na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wa Idara ya Mapato katika halmashauri ili kufanya ukaguzi kwenye maeneo ya biashara.

Ameagiza ukaguzi huo ufanyike ili kuhakikisha risiti za elektroniki (EFD) zinazotumika ni zile zinazotokana mashine zilizothibitishwa na kusajiliwa.

"Ni muhimu kila kiongozi anayehusika ashiriki katika kuhamasisha matumizi ya mashine za EFD na kufuatilia hali ya utoaji wa risiti kwa nidhamu kubwa bila kusababisha usumbufu na kero kwa wafanyabiashara," aliagiza.

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo juzi wakati wa Kilele cha Maonesho ya Juma la Utalii na Uchumi wa Bluu yaliyofanyika wilayani Mafia, mkoani Pwani.

Hatua hiyo imekuja baada ya kubainika kuwapo watu wanaojihusisha na biashara ya kuuza risiti za EFD kwa wafanyabiashara au watu walionunua bidhaa bila risiti.

Waziri Mkuu alisema jambo hilo ni ukiukwaji wa sheria na matakwa ya kufanya biashara nchini, hivyo akaitaka TRA iendelee kusimamia sheria, kanuni na taratibu za nchi na kuhakikisha kila mfanyabiashara anafanya biashara kwa mujibu wa sheria.

Pia aliagiza TRA iendelee kutoa elimu na kuhamasisha matumizi sahihi ya mashine za risiti za EFD.

"Ndugu wananchi, kila unapokwenda kununua bidhaa yoyote dukani na maeneo mengine, hakikisha unapata risiti inayotoka katika mashine iliyothibitishwa.

Tunaendelea kufanya ukaguzi," alisema.

Majaliwa aliagiza TRA ihakikishe inafuatilia kikamilifu wateja wanapewa na kudai risiti za EFD kwa nidhamu kubwa bila kusababisha usumbufu au kero kwa wafanyabiashara na wateja kwa ujumla.

Waziri Mkuu alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kunakuwa na mazingira rahisi yatakayowawezesha wafanyabiashara wa ndani na nje kufanya biashara zao.

Aliwataka wakuu wa wilaya nchini waimarishe Mabaraza ya Biashara katika wilaya zao pamoja na kukutana na wafanyabiashara na kusikiliza changamoto zao na ushauri wao ili biashara zifanyike kwa ufanisi zaidi.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu amewataka viongozi wa mkoa wa Pwani na Wilaya ya Mafia waweke mikakati ya kuongeza kasi ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko katika maeneo yao ili kuongeza idadi ya watalii.

"Mkoa uweke mkakati wa uwezeshaji wa wananchi wanaofanya shughuli za uchumi wa buluu, Serikali ya Mkoa na Wilaya wasaidieni vijana na wajasiriamali wengine kupata fursa za elimu na mikopo ya kuendesha shughuli za biashara," aliagiza.

Waziri Mkuu pia alitumia fursa hiyo kuwasisitiza Watanzania kujenga utamaduni wa kufanya utalii wa ndani.

"Tembeleeni Mafia mjionee uzuri uliopo. Tembeleeni na vivutio vingine, niwahakikishie kuwa gharama kwa wazawa katika vivutio vyetu vya utalii ziko chini ili wananchi waweze kumudu. Wekeni utaratibu wa kutunza akiba mpate fursa ya kutembelea vivutio vilivyopo nchini," alishauri.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Tembo Nickel yapongezwa uhamishaji watu, makazi viwango kitaifa na kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa amefurahishwa na maendeleo wa Mpango wa Uhamishaji Watu na Makazi wa Tembo Nickel kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na vya kimataifa ili kuhakikisha haki inaheshimiwa na kulindwa kwa waguswa wa mradi huko Ngara.

"Nimefurahiswa kujua kwamba waguswa wa mradi watepewa fidia zao kwa namna ambayo haitawaacha maskini. Utataratibu wa kuweka asilimia 100 ya fedha kwenye akaunti zao za benki, lakini kukiwa na kikomo cha kutoa hadi asilimia 60 kabla uhamisho kwenye maeneo mbadala na asilimia 40 baada ya uhamisho, utatoa usalama wa kutosha," alisema Dk. Kiruswa.

Kaya 336 zinazoguswa na mradi zitahamishwa kwenye maeneo mbadala kwenye vijiji saba vya karibu, na watachagua wenyewe kupitia njia ya kura. Kampuni itawajengea nyumba mbadala na kuhakikisha wanarejesha uchumi wao. Kwa sasa mradi uko mbioni kuzindua kampeni ya fursa kwa wazawa mwezi huu kusajili ujuzi na watoa huduma ili mchango wa wenyeji utambuliwe na kutumika na mradi na kuendana na ahadi za serikali kwa maendelo ya nchi.

Kampuni ya Tembo Nickel inataka kuendesha mradi kwa njia endelevu zaidi na imeomba Wizara ya Madini isaidie uboreshaji wa miundombinu, hususan barabara ya vumbi ya kilometa 80 kutoka eneo la mradi hadi Mizani Murusagamba ambayo inatarajiwa kutumika wakati shughuii za ujenzi zitakapo ongezeka na wakati shughuli za uchimbaji wa madini zitakapoanza.

"Hiyo ndio njia fupi inayopendekezwa kwani itakuwa na ufikaji wa moja kwa moja kwenye kiwanda cha kusafisha haya madini huko Kahama, hii ikiwa njia ambayo haina watu wengi. Sitaraji kuwa katika hali ya sasa ya barabara, itaweza kuhimili idadi ya magari itakayo ongezeka tukianza ujenzi wa awali katikati ya mwaka ujao. Tunakadiria hadi malori 40 kwa siku," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tembo Nickel, Benedict Busunzu.

Naibu Waziri alisisitiza ushirikiano wa serikali ili mradi uanze kwa wakati.

"Tunaelewa umuhimu wa barabara hii na lazima tuipe kipaumbele, hatutaki hiki kiwe kikwazo katika kufanikisha huu mradi. Nina nia ya kumshirikisha Rais kwenye suala hili ili tuweza kulipatia ufumbuzi kwa wakati kwa pamoja. Nina hakika kwa umuhimu wa huu mradi wa kimkakati, suala hili litashughulikiwa kwa uharaka wake, pamoja na suala ya nishati," alisisitiza Dk. Kiruswa.

Tembo Nickel Corporation Limited (Tembo Nickel) ni kampuni itakayochimba na kusafisha madini na kuundwa kwa mkataba wa ushirikiano baina ya Kabanga Nickel limited (asilimia 84) na Serikali ya Tanzania (asilimia 16) kwa uendelezaji wa



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tembo Nickel, Benedict Busunzu akizungumza na Naibu Waziri wa Madini, Steven Kiruswa, alipotembelea eneo la mradi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima alizeti waomba kubadilishiwa mbegu

**Na Elisante John,** SINGIDA

BAADHI ya wananchi wa Kata ya Ngimu, Halmashauri ya Wilaya ya Singida, wameiomba serikali kuwapatia wakulima aina mpya ya mbegu ya alizeti, itakayouzwa kwa bei nafuu ya ruzuku, ili iwaletee tija zaidi, wadau wote wa kilimo nchini.

Msimu wa 2022/2023, serikali iligawa mbegu aina ya Record kwa ruzuku ya Sh. 5,000 kwa kilo moja, baada ya wakulima msimu wa 2021/2022, kuilalamikia serikali kuhusu mavuno haba, wakidai yalitokana na mbegu dhaifu, iliyotolewa pia na serikali wakati huo, kwa bei nafuu.

Mmoja wa wakulima hao, Mwajuma Salim, alisema mbegu hiyo haifai kutokana kutoa mavuno haba yanayofikia magunia mawili mpaka matatu kwa ekari moja na hata ikichakatwa huzalisha chini ya lita 17 za mafuta, wakati Haysan hutoa mafuta zaidi ya lita 25, kwa ujazo unaofanana, kwa gunia la ujazo wa kilo 60 hadi 65.

"Tunaomba serikali itubadibadilishie mbegu ya alizeti, hii ya msimu uliopita haifai, wasituletee mbegu bila ya kutushirikisha sisi wakulima...nimelima ekari nne, lakini nimevuna magunia mawili, hapo sasa kweli hii ni mbegu bora," alihoji Mwajuma.

Akizunggumzia tatizo hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya uwajibikaji na ufuatiliaji (SAM), Kata ya Ngimu, Issa Ng'imba, alisema mbegu aina ya Record, ikiota shambani, hukua ikiwa na matawi mengi yasiyo na faida, huku ile ya Haysan hustawisha na tawi lenye sahani moja na mbegu zake nyingi, hivyo huleta tija kiuchumi.

Kutokana na hasara waliyopata, mwenyekiti huyo ameiomba Serikali isamehe wakulima rejesho la fedha za ruzuku, kutokana na mbegu walizokopeshwa kuwatia hasara.

Aidha, Ng'imba ameiomba serikali kusitisha msako kwa waliokwama kurejesha, kutokana na baadhi ya vijana wa kijiji hicho kuanza kujificha na kukosa uhuru wa kutembea, kwa sababu ya kusakwa na askari mgambo.

Mkulima mwingine wa kijiji cha Ngimu, Emmanuel Mungwe, aliiomba serikali kupeleka wataalamu, kupima afya ya udongo, ili kuleta tija kiuchumi, kwa jamii husika.

Mwenyekiti wa kitongoji cha Madukani, kijiji cha Ngimu, Richard Hango, pamoja na kukiri msako kwa ambao hawajarejesha deni la ruzuku serikalini, aliungana na madai ya wakulima mbegu ya mkopo, msimu uliopita hazikuwa na tija.

Pia, ameiomba serikali ipunguze bei ya mbegu aina ya Haysan inayohitajika sasa kwa wakulima, na iuzwe kwa bei ya ruzuku, badala ya Sh. 48,000 kwa kilo, hali inayowalazimu baadhi ya wakulima kuuza mbuzi na bado fedha inayopatika inakuwa haikidhi hitaji la shamba.

Aliiomba serikali kupeleka mbolea ya kutosha kwa bei ya ruzuku, ili mkulima aweze kunufaika na uzalishaji wa mazao, kupitia mbolea itakayouzwa kwa bei nafuu kwenye maeneo ya vijijini.

Mkuu wa idara ya Kilimo, uvuvi na mifugo, Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Nathalia Mosha, alikiri baadhi ya wakulima kulalamikia mavuno duni ya alizeti msimu ulioisha 2022/23, kupitia mbegu hizo.

Alifafanua kuwa, kuna baadhi ya maeneo kulingana na udongo wa sehemu husika, wakulima walipata mavuno ya kutosha kupitia mbegu aina ya Record.

Mosha alisema serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Singida, imenunua mashine maalumu kwa ajili ya kupima afya ya udongo na anaamini tatizo hilo linakwenda kwisha kuanzia msimu ujao wa kilimo.

Kuhusu wakulima kupatiwa mbegu ya ruzuku aina ya Haysan, Mosha alifafanua kuwa halmashauri ya wilaya, imewasilisha ombi serikalini tangu msimu ulioisha wa kilimo, lakini wanasubiri uamuzi kutoka kwenye mamlaka husika zinazosimamia kilimo, nchini.

Kwa mujibu wa Katibu Tawala Msaidizi, Uchumi na Uzalishaji, Stanslaus Choaji, kupitia Kikao cha Kamati ya Ushauri, Mkoa wa Singida cha Machi mwaka huu,

Mkoa wa Singida msimu 2022/23, ulipokea mbegu ya ruzuku kwa zao la alizeti aina ya Record CI kutoka ASA, tani 395.38, kati ya 1,262.5 zilizoombwa, huku Halmashauri ya Wilaya ya Singida, ikipokea zaidi ya tani 67 kati ya zilizohitajika.

## Mwanafunzi wa kitanzania aibuka mshindi wa pili shairi lugha kihindi

**Na Romana Mallya**

KITUO cha Utamaduni wa India Swami Vivekananda (SVCC) kwa kushirikiana na ubalozi, wamesherehekea maadhimisho ya Lugha ya Kihindi huku mwanafunzi wa kitanzania akiibuka mshindi wa pili wa uandishi bora wa shairi kwa lugha ya taifa hilo.

Mwanafunzi huyo ni Ramadhan Lingwele wa Kidato cha Pili katika Shule ya Sekondari ya Nzasa ni miongoni mwanaojifunza lugha ya Kihindi kituoni hapo kila wiki.

Maadhimisho hayo yalifanyika mwishoni mwa wiki katika kituo hicho mkoani Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wana diaspora wa India pamoja Watanzania ambao walionyesha umahiri wao katika kuzungumza lugha hiyo na kucheza na kuimba nyimbo za utamaduni wa taifa hilo.

Balozi wa India nchini, Pradhan Binaya, alizungumzia wanavyojivunia lugha ya taifa lao na kuhamasisha makundi mbalimbali kujifunza Kihindi.

Kwenye kituo hicho kila wiki vijana wa kitanzania wa kike na wakiume huenda kujifunza lugha hiyo na miongoni walioshiriki kuzungumza Kihindi, kucheza nyimbo za utamaduni wa taifa hilo, ni wanafunzi wanaosoma kituoni hapo.

Lingwele alisema hii ni mara ya pili kushinda nafasi ya pili ya uandishi wa mashairi akiwa kati ya wanafunzi 60 walioshiriki.

"Ninajivunia kujifunza lugha ya Kihindi. Ninapenda kujifunza lugha mbalimbali za kimataifa ninajua mbali ya kuwa kivutio ni fursa ya pekee hata katika ajira.

"Nilijiunga hapa mwaka juzi baada ya kaka yangu ambaye yeye alinitaangulia hapa na kunihamasisha kuja kujifunza, huwa ninakuja hapa kituoni kila wiki na kuungana na vijana wenzangu wa kitanzania kujifunza Kihindi.

"Kwa sasa ninajua kuzungumza kidogo, ninaamini baada ya muda nitajua zaidi. Fursa nyingine zinazotolewa ni kuimba, kucheza na mambo mengine ya utamaduni wa India," alisema.

Alisema vijana walio katika hali ya umaskini hukosa fursa kama hizo kwa sababu ya kutojichanganya. Akizungumzia shairi lililompa ushindi alisema linamwelezea mtu ambaye anatoa msaada halafu anakwenda kujitangaza sehemu kwamba 'bila mimi, asingefanikiwa'.

"Nimeonyesha kwamba mtu wa namna hii ambaye ametoa sadaka kwa mtu au watu na kujitangaza, sadaka yake haitakubaliwa na Mwenyezi Mungu.

"Hapa tunapewa elimu bure na kama hivi nilivyoshinda, nimepata fedha na huwa pia wanatoa fursa za kujifunza nchini kwao na kuna programu ya muziki kwa wenye kipaji cha kuimba, kucheza nyimbo za utamaduni wao na kuchora," alisema.

# Atuhumiwa kuishi kinyumba na mama, watoto wawili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MATUKIO ya ukatili wa kijinsia yanazidi kuitesa Kata ya Mwika Kaskazini, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, baada ya safari hii mpagazi mmoja (jina limehifadhiwa), akituhumiwa kuishi kinyumba na mama na wanawe wawili wa kike kama wake zake.

Kati ya wake zake hao ambao ni ndugu wa familia moja, yumo mwanafunzi wa kidato cha nne wa miaka 17, ambaye anasoma katika Shule ya Sekondari Lyakrimu.

Mpagazi huyo anayefanya kazi ya kubeba mizigo ya watalii katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, alikuwa akifuatiliwa nyendo zake na wanaharakati wanaofanya kazi na mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya watoto na wanawake.

Mradi huo unaoendeshwa na Shirika la KWIECO kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT Trust).

Akizungumzia ukatili huo mwishoni mwa wiki, wakati wa kikao kazi cha tathmini ya kupitia utekelezaji wa mradi huo, mwanaharakati, Dorcas Mringo, alisema aliyeibua sakata hilo ni baba mzazi wa watoto hao, ambaye aliumizwa na uamuzi huo uliokatisha ndoto za masomo za watoto wake.

"Katika kijiji chetu tumekutana na kisa na mkasa wa mama mmoja (jina limehifadhiwa) alikuwa na uhusiano wa kingono na porter (mpagazi) na alipomchoka akaamua kumwozesha binti yake mkubwa ambaye amekaa na huyo mtuhumiwa miaka mitatu bila kupata mtoto.

"Baada ya binti wa kwanza kushindwa kushika ujauzito, mama akamwozesha tena binti yake wa pili ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Lyakrimu anayetarajiwa kufanya mitihani ya taifa, wakati wowote kuanzia sasa."

Inaelezwa kuwa, baada ya binti huyo wa kidato cha nne kukatisha masomo yake kutokana na ujauzito, baba yake alifuatilia kujua kwa nini mwanae haendi shule na alipogundua alikimbilia kutoa taarifa kwa wanaharakati hao wa haki za binadamu.

"Baba alilia kutokana na wanawe kuozeshwa katika umri mdogo, akdai kufichwa juu ya ndoa hiyo ya ndugu wa familia moja. Tumemshirikisha kisa hiki Mratibu wa Elimu Kata na Ofisa Mtendaji wa Kata na tumemkamata mtuhumiwa na kumkabidhi polisi," alisema.

Akifafanua zaidi juu ya ukatili huo, mwanaharakati Easther Mlay, alisema mtuhumiwa baada ya kufikishwa polisi, akiwa mbele ya OCS (Mkuu wa Polisi wa Kituo) Himo, alikiri mama huyo ni mkewe wa kwanza na watoto wake hao wawili wa kike pia ni wake zake

Kwa mujibu wa Easther, binti huyo wa kidato cha nne alipopelekwa kufanyiwa uchunguzi wa afya kwenye Kituo cha Afya, aligundulika kuwa na ujauzito wa miezi mitatu.

Mratibu wa mradi huo wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya watoto na wanawake, Veronica Ullomi, alisema mradi huo unalenga kuchangia uboreshaji wa msaada wa kisaikolojia, haki ya kielimu na kumaliza matatizo ya kiakili yanayohusiana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto mkoani Kilimanjaro.

Pia, unalenga kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto kwa kuimarisha afya ya akili kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, inayohusiana na ukatili kwa wanawake, wasichana, watoto na makundi mengine ya pembezoni na wale walioathiriwa na vikwazo vya unyanyasaji wa kitamaduni na mijadala katika jamii za vijijini na mijini.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua gwaride la wahitimu wa Jeshi la Uhamiaji katika Chuo cha Uhamiaji cha Raphael Kubaga kilichopo wilayani Mkinga mkoani Tanga juzi, alikuwa mgeni rasmi na kufunga mafunzo hayo ya awali namba 1, 2023. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Watoto mil.1.7 kufikiwa na mpango uboreshaji maisha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHIRIKA la Compassion International Tanzania, limezindua mpango mkakati wa miaka mitano ambao utawafikia watoto milioni 1.7 wenye uhitaji wa kuchangia na kuboresha maisha yao.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Mkurugenzi wa shirika hilo, Mary Lema, wakati wa uzinduzi wa mpango huo.

Alisema tangu kuanzishwa kwa shirika hilo mwaka 1999 limekuwa moja kati ya mashirika makubwa ya kikristo yaliyoleta maendeleo nchini na wanafanya kazi na makanisa washirika wenza katika mikoa 21 ya Tanzania Bara kwenye halmashauri zaidi ya 80.

Alisema wanafanya kazi na makanisa zaidi ya 550, huku zaidi ya watoto 115,000 wakifadhiliwa kupitia miradi inayolenga kuboresha afya na lishe ya mama na mtoto, elimu, maishilio, uzalishaji, maji na usafi wa mazingira.

"Ni siku yenye umuhimu mkubwa kwetu tunapokusanyika pamoja kuzindua mkakati wa miaka mitano wenye mabadiliko na matamanio makubwa ambao tumeuita kwa ufasaha 'Ahadi kwa Jirani Yetu," alisema.

Vilevile alisema mpango huo wameuandaa kwa kuzingatia takwimu za kitaifa, walitumia takwimu mahususi walizozipata kwa kushirikiana na serikali.

Naye Kamishna wa Ustawi wa Jamii, kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wanawake na Makundi Maalum, Dk.Nandere Mhando, alisema huduma za kijamii hutolewa kwa mtu mmoja, familia, makundi mbalimbali na jamii kwa ujumla.

Alisema lengo la kutoa huduma hizo ni kutatua matatizo katika kijamii ili kuboresha ustawi wao kiakili, kimwili, kihisia, kijamii na kimaadili. Kadhalika alisema huduma za ustawi wa jamii zinalenga kusaidia na kuwezesha makundi maalum kushiriki kikamilifu katika shughuli za ustawi na maendeleo ya kijamii.

Alisema wizara inaendelea na utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi kupitia serikali za mitaa kwenye halmashauri zote.

Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika hilo, Dk. Elieshi Kisinza, alisema katika mpango mkakati huo kuna ahadi ya kuhakikisha kila mtoto anapata nafasi ya kustawi, kupendwa na kulindwa.

# Majaliwa atoa maagizo uboreshaji Chuo cha Uhamiaji

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maagizo kwa uongozi wa Mkoa wa Tanga kuboresha miundombinu ya Chuo cha Uhamiaji cha Raphael Kubaga kilichopo wilayani Mkinga pamoja na kusisitiza mambo kadhaa kwa wahitimu wa mafunzo ya awali ya jeshi hilo.

Alitoa maagizo hayo jana mkoani hapa wakati akifunga mafunzo ya awali kozi namba 1, 2023 katika viwanja vya chuo hicho ambacho kilifunguliwa rasmi mwaka 2020, lakini miundombinu yake bado haijakamilika.

Majaliwa alizitaka mamlaka za maji, Tanga- Uwasa pamoja na Ruwasa wilayani hapa mkoa kuhakikisha wanafikisha huduma ya maji yenye uhakika wa kupatikana wakati wote.

Pia aliiagiza TARURA kuangalia jinsi ya kufanya matengenezo na kuweka lami kwenye barabara inayokwenda chuoni hapo kutoka Barabara Kuu ya Horohoro.

"Nimesikia kero zenu hapa chuoni, kwanza barabara inayoingia chuoni kutoka barabara kuu, lakini pia za humu ndani pamoja na uwanja wetu wa gwaride havina lami, nianze kumuelekeza Meneja wa TARURA Mkoa wa Tanga pamoja na Wilaya ya Mkinga kutengeneza barabara inayoingia kwenye chuo chetu kwa kiwango cha lami," alisema Majaliwa.


Eneo lingine lenye kero ni kuhusu ukosefu wa jengo la mama na mtoto hapa chuoni ambapo Majaliwa alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha wanaiingiza zahanati hiyo katika migawo ya vituo vya afya ambavyo vinatoa huduma hiyo ili wanakijiji wanaokwenda kupata tiba waweze kupewa huduma stahiki.

Aidha, alimwagiza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, kuhakikisha anaongea na Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba ili kuweza kukamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba za maofisa wa uhamiaji zikiwemo za wakufunzi ambazo zinahitajika zijengwe kwenye eneo hilo.

Pia, alitoa msisitizo kwa wanafunzi waliohitimu mafunzo yao kwenda kuyatumia vema katika kudhibiti wahamiaji wanaoingia nchini.

Alisema: "kufuatia kuongezeka kwa teknolojia za kisasa na makosa mbalimbali ya kiuhalifu husani biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, kila mmoja ahakikishe kwamba anapata maarifa mapya mara kwa mara ili aweze kukabiliana na mabadiliko hayo."

Alisisitiza kwamba ili kuondokana na tatizo la kusambaa kwa vitambulisho vya taifa kama ambavyo vilisambaa vya mpigakura ni lazima nchi kuwa makini na kufanya uhakiki wake ili kuwawezesha wananchi wote ambao wana uhalali wa kuwa na vitambulisho hivyo waweze kuvipata.



## HABARI KANDA YA ZIWA



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, akimsikiliza Meneja Mauzo wa Kampuni ya Almansour Auto Ltd, wauzaji wa magari ya Isuzu alipokagua banda lao kabla ya kuyafunga maonyesho ya madini mkoani Geita juzi. Katikati ni Meneja Masoko wa kampuni hiyo, Ndeshi Rajabu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baada ya kutembea umbali mrefu, wanafunzi wajengewa madarasa

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

KAMPUNI ya madini ya Sotta (SMCL) imejenga vyumba vinne vya madarasa pamoja na ofisi mbili za walimu kwa ajili ya shule mpya ya sekondari katika Kijiji cha Lubungo mkoani Mwanza.

Uamuzi wa kujenga madarasa hayo ni kuwaondolea adha wanafunzi katika Kijiji hicho waliokuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma ya elimu.

Ujenzi wa shule hiyo pia ulishirikisha wananchi, ulianza Julai 2023 na kukamilika Septemba umegharimu Sh.milioni 38.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa mradi huo, Meneja Uhusiano wa kampuni hiyo, John Bwana, alisema hatua hiyo ni sehemu ya mpango wa uwezeshaji jamii na kuongeza mahusiano ya karibu.

Alisema katika mradi huo wananchi walitoa ardhi kupitia serikali ya mtaa pamoja na kushiriki katika ujenzi wa msingi hadi kwenye lenta, kampuni hiyo kumalizia ujenzi wake kwa kushirikiana na Shirika la Wazalendo Group.

Naye Ofisa Mkuu wa Fedha kutoka SMCL, Isaac Lupokela, alisema wataendelea kushirikiana na serikali katika kuboresha miundombinu na ubora wa elimu.

"Vilevile tutatoa madawati 160 katika shule hii pamoja na miche ya miti ili kuendelea kutunza mazingira na kuifanya shule iendelee kuwa nadhifu na kuvutia kwa wakati wote," alisema Luokela.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Sengerema, Cuthbert Midala, akizungumza baada ya kukabidhiwa majengo hayo aliipongeza kampuni hiyo na kuiomba kuendeleza ushirikiano katika maeneo yenye uhitaji.

"Tunategemea ushirikiano mkubwa kutoka SMCL kwani ni kampuni ya ubia kati ya serikali inayomiliki asilimia 16 na Kampuni ya Nyanzaga inayomiliki aslimia 84," alisema.

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Sengerema, Genoviva Chuchumba, alisema kukamilika kwa shule hiyo kutasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Ngoma yenye wanafunzi 1,220.

## Waendesha baiskeli kwenda Butiama kumuenzi Hayati Nyerere

**Na Mwandishi Wetu,** BUTIAMA

MSAFARA wa waendesha baiskeli 200 unaojulikana kama 'Twende Butiama' umeanza rasmi safari ya kuelekea Butiama katika makazi ya Baba wa Taifa, Hayati Julius Nyerere, wanatarajia kuwasilia Oktoba 14.

Lengo la safari hiyo ni maadhimisho ya kumbukumbu ya kifo kumuenzi Hayati Nyerere ambaye alifariki dunia Oktoba 14, 1999.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, Ofisa wa Michezo katika Baraza la Michezo la Taifa, Benson Chacha aliwapongeza waandaaji wa Twende Butiama pamoja na wadhamini wa msafara huo, Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation kwa jitihada za kufanikisha tukio hilo.

"Nichukue fursa hii kuwapongeza waandaji na washiriki wote wa msafara ambao wana dhamira ya dhati ya kumuenzi Baba wa Taifa. Tukio hili siyo linaendea kuchagiza shughuli mbalimbali ambazo Mwalimu Nyerere alikuwa anazipa kipaumbele lakini pia zitahamisisha Watanzania kupenda michezo," alisema.

Aliongeza kuwa dhumuni ya msafara wa huo ambao utakuwa na waendesha baiskeli takribani 200 watakaoendesha kilometa 1,500 na kupita kwenye wilaya 20 ndani ya mikoa 10.

Msemaji wa familia ya Mwalimu Nyerere, Waziri Mkuu Mstaafu, Joseph Warioba alisema: ..."Nimefurahi kuona tukio hili limeweza kukusanya nchi tofauti zikiwamo za Afrika ya Mashariki kitu ambacho kinaonyesha mshikamano wetu. Njiani mtakapopita mtaweza kujionea nchi yetu ya Tanzania kwa upana wake na kupitia shughuli mtakazozifanya njiani zitawanufaisha Watanzania".

Mwenyekiti wa Vodacom Tanzania Foundation, Harriet Lwakatare alisema: "Kama tulivyoeleza wakati wa uzinduzi wa ushirikiano wetu, tuna imani kubwa na Twende Butiama husussani kwa kile wanachokifanya katika kuenzi maisha na urithi wa Hayati Nyerere.

## Maofisa nyuki wamepewa pikipiki kufuatilia miradi

**Na Halima Ikunji,** UYUI

TAASISI ya Enabel ya nchini Ubelgiji inayojihusisha na miradi ya utunzaji mazingira na ufugaji nyuki katika mikoa sita nchini imekabidhi pikipiki 15 zenye thamani ya Sh. milioni 131.4 kwa maofisa ufugaji nyuki mkoani hapa.

Akizungumza juzi katika hafla ya kukabidhi vitendea kazi hivyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mkuu wa Wilaya ya Uyui, Zakaria Mwansansu, alisema vifaa hivyo ni muhimu sana kwa kuwa vitawarahisishia kazi ya ufuatiliaji miradi hiyo.

Alibainisha kuwa pikipiki hizo zimetolewa katika wilaya 15 zinazotekeleza Mradi wa Kuboresha Mnyororo wa Thamani ya Ufugaji Nyuki (BEVAC) unaotekelezwa katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi, Singida, Shinyanga na Pemba. Mwansansu aliongeza kuwa katika kuchochea mafanikio makubwa ya mradi huo wafuga nyuki 1,947 wamepewa mafunzo ya ufugaji bora na uchakataji mazao ya nyuki.

Alisisitiza kuwa mafunzo hayo ni endelevu na vifaa walivyopewa ni chachu ya kuleta tija kwenye uzalishaji na uboreshaji wa mnyororo wa thamani na kupelekea kuongezeka kwa mapato ya mazao ya nyuki katika mikoa hiyo.

Meneja Miradi wa Enabel, Martin Mgallah alisema mradi huo unaotekelezwa na shirika hilo kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) umelenga kuinua uchumi wa jamii ya wafuga nyuki wote walioko katika wilaya na mikoa husika. Aliongeza kuwa mbali na kutekelezwa katika mikoa mitano ya Tanzania Bara mradi huo pia unatekelezwa visiwani Pemba ili kuongeza mnyonyoro wa thamani katika sekta ya ufugaji nyuki.

Mwakilishi wa EU, Cedric Merel alisema pikipiki hizo zitachochea maendeleo ya sekta ya ufugaji nyuki nchini, ikiwemo kuongeza ufanisi na kuinua uchumi wa taifa.

## Soko lililokosa choo muda mrefu hatimaye chajengwa

**Na Jenesta Jasson,** MISSENYI

OFISA Mtendaji wa Kijiji cha Mtukula Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, Mwanamkuu Waziri, ametoa onyo kwa wafanyabiashara na wananchi katika Soko la Mtukula kuacha kuchafua mazingira, hali inayohatarisha mlipuko wa magonjwa.

Soko hilo lililopo mpakani mwa Tanzania na Uganda linadaiwa kutokuwa na choo kwa ajili ya wafanyabiashara na wateja sokoni hapo hali ambayo imekuwa ikisababisha baadhi yao kujisaidia katika mifuko.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka kutafuta mahali sahihi kwa ajili ya kujihifadhi wakati shughuli za ukarabati wa choo cha soko hilo ambao umeanza kufuatia agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ukiendelea.

"Naishukuru serikali kupitia Waziri Mkuu kwa kuliona tatizo hili na kulifanyia kazi, kwa sasa ukarabati unaendelea na niwaombe wananchi kuwa wavumilivu na kutumia choo kilichopo katika eneo la stendi wakati tukimalizia ukarabati," alisema.

Nao baadhi ya wajasiriamali katika soko hilo waliishukuru serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu aliyetoa agizo la ujenzi wa choo hicho kwani hawakuwa na choo jambo lililosababisha uchafunzi wa mazingira.

Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, Godson Ngaleo, alisema ukarabati wa vyoo hivyo umeanza na utagharimu Sh.milioni sita na unatarajia kukamilika ndani ya wiki moja.

Nipashe
Spotika



FARASI WA3 WAKUCHUNGWA LIGI YA MABINGWA ULAYA MSIMU HUU UK. 12-13



# TIMU 4 ZINAZOWEZA KUBEBA UBINGWA WA EPL MSIMU HUU

Kikosi cha Manchester City

**LONDON,** England

TUKIENDA kwenye kiwango cha ushindani, Ligi Kuu England (EPL), ni moja ya ligi ngumu kutabirika na kuchambua matokeo yake.

Kuna timu nyingi za chini ambazo zinaweza kuzisumbua timu kadhaa zenye majina makubwa wakati wa kampeni.

Hili limethibitishwa huku tukishuhudia jinsi Newcastle United na Brighton & Hove Albion zilivyotawala timu kadhaa zenye majina makubwa msimu uliopita.

Hata hivyo, timu kadhaa kama vile Manchester City, Tottenham Hotspur na Liverpool zimeanza msimu mpya kwa kasi kubwa. Lakini Man City Jumamosi ilishuhudiwa ikisulubiwa na Wolves kwa mabao 2-1 kama ilivyokuwa kwa Liverpool ikiadhibiwa na Spurs kwa idadi hiyo ya mabao.

Makala haya yanaangalia timu nne zinazopewa nafasi kubwa kushinda taji la Ligi Kuu msimu huu, haya sasa...

**#4. Tottenham Hotspur**

Tottenham Hotspur ingependa kuweka msimu uliopita nyuma yao. Hawakuwa kwenye kiwango kizuri katika mashindano yote na pia walishindwa kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, mabadiliko katika maeneo kadhaa ya klabu yanaweza kuonekana kama pumzi ya hewa safi imeongeza kwenye kikosi. Ingawa ilionekana kuwa kuondoka kwa Harry Kane kungeiathiri Spurs, timu hiyo haikuhisi kukosekana kwake.

Spurs wamesajili pointi 17 katika mechi saba za ligi, na kwa sasa wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo.

Wakati timu hiyo haikusajili wachezaji wengi wenye majina makubwa, usajili wa James Maddison pamoja na mwanzo wao mzuri umewafanya kuwa miongoni mwa timu zinazotakiwa kuangaliwa sana. Ingawa ni mapema kutabiri, wana nafasi nzuri ya kushinda taji lao la kwanza la Ligi Kuu ikiwa wataendelea kwa njia hiyo hiyo.

**#3. Arsenal**

Wakiwa wameshindana vikali na Manchester City msimu uliopita, 'Washikabunduki' hao bila shaka ni miongoni mwa timu zinazopewa nafasi kubwa kushinda taji msimu huu. Wameanza msimu wao kwa kiwango kizuri kwani wamesajili pointi 17 sawa na Spurs katika mechi saba za ligi.

Kusajiliwa kwa wachezaji kadhaa wa daraja la juu kama Declan Rice, David Raya na Jurrien Timber kumewaongezea nguvu. Uchovu wa kikosi ndio sababu kuu iliyowafanya Man City kuwazidi nguvu kwenye mbio za ubingwa kampeni zilizopita.

Kwa hiyo, kwa kuzingatia kiwango chao cha sasa na uimara wa kikosi, wana nafasi nzuri kwenye ubingwa wa Ligi Kuu.

**#2. Liverpool**

Jurgen Klopp alikuwa chini ya uangalizi mkubwa msimu uliopita huku timu yake ikishindwa kujisajili kuwa moja ya timu zilizotawala dimba kwenye Ligi Kuu.

Hii ilisababisha kuimarika kwa kikosi hicho jambo ambalo limekuwa na matokeo chanya katika utendaji wa timu.

Kwa sasa 'Wekundu' hao wanashika nafasi ya nne kwenye msimamo wakiwa wamejihakikishia pointi 16 kutokana na michezo yao saba ya kwanza ya ligi.

Inaweza kubishaniwa kuwa ni mapema sana kusifu kikosi. Hata hivyo, kusajiliwa kwa viungo kadhaa wa daraja la juu kama Ryan Gravenberch, Dominik Szoboszlai na Alexis Mac Allister kumewapa uwiano unaohitajika katika safu ya kiungo.

Ukosefu huu wa usawa ulikuwa mojawapo ya sababu kwa nini timu ilijitahidi katika kampeni iliyopita.

Ingawa changamoto hizo zimeshughulikiwa, Wekundu hao wana uwezekano mkubwa wa kutwaa taji la Ligi Kuu England iwapo wataendelea kuwa kwenye kiwango cha sasa.

**#1. Manchester City**

Inaonekana kana kwamba Man City hawarudi nyuma hivi karibuni. Ndio timu pekee ya Ligi Kuu ambayo ilisajili mfululizo wa ushindi wa asilimia 100 kwenye ligi msimu huu baada ya mechi sita kabla ya juzi Wolves kuwatibulia kwa kuwachapa mabao 2-1.

Wengi walitarajia timu ya Pep Guardiola kukabiliwa na matatizo, kwani nyota wake wa kikosi cha kwanza kama Riyad Mahrez na Ilkay Gundogan waliihama klabu hiyo msimu uliopita wa majira ya joto.

Vile vile, jeraha la Kevin De Bruyne lilitarajiwa kwa kiasi kikubwa kuwa na athari mbaya kwenye safu ya kiungo, lakini timu imekabiliana bila watu wao muhimu. Sababu hizi zinaonesha jinsi kikosi kilivyo na nguvu na uwezo, na hii pia ni ishara kwamba timu iko thabiti kama kawaida.

Wakiwa wamesajili pointi 18 kutoka kwa mechi saba za ligi, hakuna shaka kuwa Man City wanabakia kuwa wagombea wenye uwezekano mkubwa wa kuibuka washindi wa Ligi Kuu kwa mara nyingine tena.

## ISIKUPITE

HADI kufikia juzi, Jumamosi jumla ya timu 11 zilishafuzu hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika ambazo ni; Al Ahly (Misri), Pyramids (Misri), Jwaneng Galaxy (Botswana), TP Mazembe (DR Congo), Petro Atletico (Angola), Esperence Tunis (Tunisia), Medeama (Ghana), Mamelodi Sundowns (Sauzi), Yanga (Tanzania), Etoile Sahel (Tunisia), Wydad (Morocco) zingine nne zilitarajiwa kujulikana jana na moja kesho.




Arteta na Arsenal wake

# FARASI WATATU WA KUCHUNGWA LIGI YA MABINGWA ULAYA MSIMU HUU

**NYON,** Uswisi

HATUA ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2023-24 ilianza baada ya mapumziko ya kwanza ya kimataifa ya msimu huu kuanzia Septemba 19.

**Baadhi ya timu bora barani Ulaya zilipangwa katika makundi ya rahisi, huku nyingine zikiwa kwenye makundi yatakayowafanya wapate ugumu wa kufuzu hatua ya mtoano.**

Miamba kama vile Manchester City, Bayern Munich na Real Madrid zinapewa nafasi kubwa msimu huu.

Ukiacha hilo pia baadhi ya washindani wa huko nyuma wa michuano hiyo kama Barcelona, Atletico Madrid na Arsenal wanaweza kusonga mbele kwa urahisi kama washindi wa kundi.

Wakati klabu nyingi kubwa zinatarajiwa kutinga hatua ya mtoano ya shindano hilo, nyingine zinaweza kujikuta kwenye wakati mgumu msimu huu.

Makala haya yanaangazia klabu tatu (farasi watatu), zinazoweza kushangaza wengi msimu huu, twende sasa...

**#3. RB Leipzig**

RB Leipzig ilipoteza vipaji vyake vingi msimu huu wa majira ya joto. Kuondoka kwa Dominik Szoboszlai, Christopher Nkunku, na mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol kunaweza kulemaza kikosi chochote.

Lakini ikiwa kiwango chao cha hivi karibuni kitaendelea ni wazi kuwa timu hiyo ya kocha Marco Rose bado ina mengi ya kutoa.

Baada ya kuichabanga Bayern Munich katika uwanja wao wa nyumbani katika Kombe la Super Cup la Ujerumani, 'Die Roten' hao walipoteza kwa urahisi mbele ya Bayer Leverkusen katika mechi yao ya ufunguzi wa msimu.

Hata hivyo, maonesho mawili ya kiwango cha juu dhidi ya VfB Stuttgart na Union Berlin yameinua kiwango chao kwa kiasi kikubwa.

Kuwasili kwa Benjamin Sesko na Lois Openda kumefidia hasara ya Nkunku, ambapo Xavi Simmons amefanya vema kuchukua nafasi ya Dominik Szoboszlai.

Uwapo wa wanakampeni wazoefu kama vile Timo Werner, Emil Forsberg, Yussuf Poulsen na Dani Olmo kumeongeza kitu kwenye mashambulizi yao ambayo tayari ni mahiri. Kampeni zao za hivi majuzi za Ulaya pia zimekuwa za kuvutia.

Walifanikiwa kutinga hatua nne za mwisho katika michuano ya Europa na Ligi ya Mabingwa Ulaya katika kipindi cha miaka minne iliyopita.

Mashambulizi yao yanaweza kuwa ndoto kwa timu yoyote barani Ulaya. Na ingawa bado haijulikani ikiwa wataweza kufidia kumpoteza Gvardiol, bila shaka wanaweza kusababisha misukosuko michache kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa kudhihirisha hilo miamba hiyo ya Ujerumani imeanza vema hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuitandika Young Boys nyumbani Uswisi kwa mabao 2-0.

**#2. Arsenal**

Baada ya kukaa kileleni mwa Ligi Kuu ya England kwa siku 248, Arteta alipoteza taji la ligi baada ya kushindwa na Manchester City.

Lakini kulingana na matarajio ya kabla ya msimu, Arsenal ilifanikiwa kufikia lengo lao kuu la msimu wa 2022-23 la kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

'Washikabunduki' hao walionesha ushindani mkubwa dhidi ya Man City na kumpata Declan Rice. Nyongeza za Jurrien Timber na Kai Havertz kwenye kikosi ambacho tayari kina vipaji inaweza kuwa mabadiliko makubwa kwao.

Ingawa kiwango cha hivi majuzi hakijawa cha kutia moyo, wanaweza kufaidika kwa kiasi kikubwa kutokana na kundi lao. Si PSV wala Lens walioshinda ligi zao msimu uliopita, huku Sevilla wakimaliza katika nafasi ya 12 kwenye LaLiga ingawa walishinda Ligi ya Europa.

Licha ya kuwa Sevilla ina wazoefu wa Ulaya, Arsenal wanapewa nafasi kubwa ya kushinda kundi hilo. Ikiwa wataepuka kushindwa dhidi ya Wahispania, wanapaswa kufuzu kama washindi wa Kundi B. Na wakifanya hivyo, wanaweza kuepukana na uzani mzito katika raundi za mapema za mtoano.

Washikabundi hao hakika wana kikosi ambacho kinaweza kutinga hatua ya baadaye ya shindano hilo. Ushindi wa msimu uliopita wa taji la Ligi Kuu ambao haukutarajiwa bado unaonesha vivyo hivyo.

Tayari Arsenal ikiwa katika Uwanja wake wa Emirates pale London, imeanza vema hatua ya makundi ya michuano hiyo msimu huu, baada ya kuitandika PSV ya Uholanzi mabao 4-0.

**#1. Napoli**

Ni kweli kwamba, Napoli wamempoteza kocha wao aliyeshinda Serie A, Luciano Spalletti, na wanaungana na Real Madrid na Union Berlin.

Lakini hawajapoteza wachezaji muhimu waliowaongoza kutwaa taji lao la kwanza la Serie A katika miongo mitatu.

Victor Osimhen, Khvicha Kvaratskhelia na Hirving Lozano wanaweza kuhatarisha ulinzi wowote barani Ulaya, ilhali uzoefu wa Mario Rui na Giovanni Di Lorenzo unapaswa kuwa muhimu.

Kikosi kilichosalia kimejaa ubora uwanjani kote, ambao utasaidiwa na ununuzi wa vijana Giacomo Raspadori na Jesper Lindstrøm.

Lakini msukumo mkubwa zaidi kwa mafanikio ya Napoli kwenye Ligi ya Mabingwa utatolewa na udhaifu wa Real Madrid.

'Los Blancos' tayari wamewapoteza Thibaut Courtois, Eder Militao, na Arda Guler kutokana na majeraha ya muda mrefu, na Vinicius Jr anaweza kubaki hafai kwa ziara ya Real huko Napoli.

Kwa hiyo, ikiwa Napoli watafanikiwa kuifunga Los Blancos huko Naples, watakuwa na nafasi kubwa ya kushinda kundi hilo.

Msimu uliopita, Napoli walifanya hivyo kwa kuifunga Liverpool mabao 4-1 kwenye Uwanja wa Diego Armando Maradona, jambo lililosababisha Liverpool kumenyana na Real Madrid katika hatua ya 16-Bora.

Napoli huenda ikawa timu bora zaidi barani Ulaya katika kipindi cha kwanza cha msimu uliopita.

Kiwango chao cha Serie A kilishuka tu baada ya kushinda taji, na ikiwa si kwa jeraha la Victor Osimhen, wangeweza kuishinda AC Milan katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa pia.

Kwa bahati nzuri, wanaweza kwenda mbali kabisa kwenye Ligi ya Mabingwa msimu huu na tayari wameanza kwa ushindi wa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Braga ya Ureno.

## Nukuu

"Kipaumbele changu kilikuwa ni nyumba yangu, familia yangu. Niliamini 'hadi kifo kitakapotutenganisha'. Niliamini ndoto hiyo na nilikuwa na ndoto hiyo kwangu, kwa watoto wangu. Wazazi wangu wamekuwa pamoja, sijui, miaka 50 na wanapendana kama siku ya kwanza, kwa upendo ambao ni wa kipekee na usioweza kurudiwa. Kwa hivyo najua inawezekana. Mama yangu haondoki upande wa baba yangu [mgonjwa]. Bado wanabusu mdomoni. Na daima umekuwa mfano kwangu. Ni kile nilichotaka kwa ajili yangu na watoto wangu, lakini haikufanyika. Ikiwa maisha yanakupa limau, lazima utengeneze limau. Hiyo ndiyo ninafanya: Kutengeneza limau," **Shakira akielezea ndoto zake zilivyokufa baada ya kuachana na nyota wa zamani wa Barcelona, Gerard Pique.**



"Tunaweza kumuuza Kai Havertz na kurudisha pauni milioni 70! Kila shabiki wa Arsenal anajua hili na nadhani tumekuwa tukijidanganya kwa muda mrefu sana kwamba tunaweza kuishi bila mmoja na ukweli ni kwamba hatuwezi," **Mchambuzi wa soka, Piers Morgan akiitaka Arsenal kumuuza Havertz Januari na kumnunua straika wa Brentford, Ivan Toney.**



"Mazungumzo mengi yatakuwa juu ya Manchester United, kuhusu wao kutotengeneza nafasi vizuri na kucheza vizuri vya kutosha, lakini Crystal Palace wanastahili sifa zote, safu yao ya ulinzi iliwazuia wenyeji kucheza. Tunajua kwamba ikiwa Crystal Palace itaweka pua mbele ni timu ngumu sana kuivunja," **Mshambuliaji wa zamani wa England na Newcastle United, Alan Shearer, baada ya United kupigwa bao 1-0 nyumbani juzi na Palace.**






Clement Mzize (wa pili kulia), akipongezwa na wachezaji wenzake wa Yanga baada ya kuifungia bao pekee dhidi ya Al-Merrikh katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Saalam juzi, wakati wakishinda 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

# YANGA YAWEKA REKODI 5 IKITINGA MAKUNDI AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

USIKU wa Septemba 30, mwaka huu utakuwa ni wa kukumbukwa kwa wanachama na mashabiki wa Yanga baada ya timu yao kufanikiwa kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara ya kwanza baada ya miaka 25.

**Wakiwa wamefurika kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam pamoja na viongozi wao wote na wale waliokuwa wakiangalia kwenye televisheni, walikuwa na furaha kubwa baada ya dakika 90 za mchezo huo kumalizika.**

Filimbi ya kumaliza mechi hiyo ilipopulizwa iliashiria mwisho wa timu hiyo kutolewa kwenye hatua za awali na raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

Ushindi wa bao 1-0 ilioupata juzi uliunganishwa na ule wa mabao 2-0 iliyoupata Septemba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Pele, Nyamirambo nchini Rwanda ukiifanya Yanga kutinga hatua hiyo kwa jumla ya mabao 3-0 dhidi ya Al Merrikh ya Sudan.

Timu hiyo ililazimika kucheza mechi zake nchini Rwanda kutokana na machafuko ya kisiasa nchini kwao, Sudan.

Zifuatazo ni rekodi mbalimbali za Yanga iliyopigana kwa muda mrefu kufika hapo ilipofanikiwa kufanya hivyo juzi...

### 1. Mara ya kwanza baada ya miaka 25

Mara ya mwisho kwa timu hiyo kutinga hatua hiyo ilikuwa ni 1998 ilipofanya hivyo kwa kuitoa Coffee ya Ethiopia kwa jumla ya mabao 8-3.

Kama ilivyofanikiwa kwenye mechi dhidi ya Al Merrikh, Yanga ilianzia ugenini nchini Ethiopia na kulazimisha sare ya mabao 2-2, ikichezwa Aprili 26, mwaka huo, zikarudiana nchini Mei 8, Yanga ikitoa kipigo cha paka mwizi cha mabao 6-1.

Na ndiyo ilikuwa timu ya kwanza nchini kutinga hatua hiyo baada ya mfumo mpya wa makundi kuanza badala ya ule wa mtoano kuanzia mwanzo hadi mwisho. Baadaye Simba ilifanikiwa kutinga makundi kwa mara ya kwanza 2003 kwa kuisukumiza nje Zamalek ya Misri.

### 2. Gamondi awapiku makocha wengine Yanga

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, pamoja na kwamba ana muda mfupi tu, lakini ameingia kwenye kitabu cha kumbukumbu cha klabu hiyo kwa kuwa ndiye kocha aliyeipeleka timu hiyo hatua hiyo baada ya muda mrefu.

Gamondi, raia wa Argentina ameichukua timu hiyo mwanzoni mwa msimu kutoka kwa Mtunisia, Nesreddine Nabi, aliyetimkia FAR Rabat ya Morocco, hivyo amelipiku kundi la makocha kutoka pembe zote za dunia ambao walikuja kuifundisha timu hiyo na kushindwa kufanya hivyo.

Kocha aliyekuwa akishikilia rekodi ya kuipeleka makundi Yanga mwaka 1998 ni Mtanzania, Tito Mwaluvanda (marehemu) ambaye vitabu vya kumbukumbu vya historia ya klabu hiyo vinaendelea kumuenzi kuwa ndiye kocha wa kwanza kuipeleka hatua ya makundi tangu ianzishwe mwaka 1935.

### 3. Timu zote ni za CECAFA

Hii ni mara ya pili sasa kwa Yanga kutinga hatua ya makundi barani Afrika, lakini katika vipindi vyote ambavyo imefanikiwa kufika imezitoa timu za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, CECAFA.

Coffee ya Ethiopia ni timu inayotoka kwenye ukanda huu, lakini Al Merrikh nayo ni timu inayotoka pia Ukanda wa CECAFA ambao Rais wake ni Wallace Karia, ambapo pia analiongoza Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini, TFF.

### 4. Yafuzu nyumbani kama Simba

Kama ilivyokuwa Simba, timu ya Yanga imeweka rekodi ya kutinga hatua ya makundi ikiwa kwenye ardhi ya nyumbani, Tanzania.

Mara zote ambazo Simba imefanya hivyo, imekuwa ikitinga ikiwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Na hata mwaka 1998, Yanga ilipotinga kwa mara ya kwanza ilifanya hivyo ikiwa nchini. Tofauti pekee ni kwamba Yanga haijawahi kutinga makundi ikiwa Uwanja wa Mkapa, badala yake Uwanja wa Taifa (Uhuru) na juzi Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

### 5. Mzize aingia kwenye rekodi

Straika Mtanzania, Clement Mzize, ameingia kwenye vitabu vya kumbukumbu kwa kufunga mabao mawili ambayo kwa kiasi kikubwa ndiyo yaliyoiwezesha kutinga hatua hiyo.

Straika huyo anayekuja juu kwa sasa, alifunga bao pekee juzi dakika ya 66 akiiwezesha Yanga kushinda 1-0.

Katika mechi ya awali nchini Rwanda alifunga bao la pili lililoinyong'onyesha Al Merrikh baada ya lile la kwanza lililofungwa na Kennedy Musonda.

Mzize pia ameweka rekodi Yanga ya kufunga bao katika mechi tatu mfululizo za Ligi ya Mabingwa. Alifunga katika mechi ya marudiano dhidi ya ASAS ya Djibouti Agosti 26, Yanga ikishinda mabao 5-1, Septemba 16 alifunga bao la pili dakika ya 78, kabla ya kufanya hivyo kwa mara nyingine tena juzi.

**JE, WAJUA?**

Premier League

KATIKA Ligi Kuu England msimu huu ni Arsenal na Tottenham Hotspur tu ndizo ambazo hazijapoteza mechi yoyote hadi sasa ikiwa ni mzunguko wa saba huku Sheffield United ikiongoza kwa kupoteza mechi nyingi zaidi (sita) ikifuatiwa na Burnley (5), Everton (5) huku Man United, Luton Town, Bournemouth na Wolverhanpton kila moja ikipoteza michezo minne.





# Watumiaji holela antibaotiki hatarini kupata usugu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Hezron Nonga, amesema matumizi holela ya dawa za antibiotiki yanachangia kwa kiasi kikubwa tatizo la usungu wa dawa kwa wanyama na binadamu.

Prof. Nonga alibainisha hayo kwenye mkutano wa siku moja uliowakutanisha wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo na taasisi zake, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Afya na wawakili wa wanyama pori.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kujadili mradi ambao utajikita katika kuangalia uelewa wa wananchi hasa wafugaji kuku kuhusu usugu wa dawa ambao hivi sasa umetoka kwa wanyama na kuhamia kwa binadamu.

Alisema mradi huo ambao utakwenda kutekelezwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Mwanza unalenga kwenda kufanya utafiti kwa wafugaji wa kuku kama wanatambua chanzo cha usugu wa dawa katika mifugo.

Kadhalika, alisema matokeo ya utafiti huo yatasaidia jamii kuwa salama dhidi ya usugu wa dawa hasa pale wafugaji watakapopunguza matumizi holela ya dawa za antibiotiki kwa kuku.

Naye Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha St. Francis Ifakara, Filbert Madoshi, alisema matumizi ya dawa yasiyo zingatia maelekezo ya wataalamu yamekuwa chanzo cha vimelea kujenga usugu wa dawa.

Alisema hivi sasa jamii imekuwa na tabia ya matumizi ya dawa ambayo hayazingatii maelekezo ya wataalamu wa afya hali ambayo kama haitafanyiwa kazi hakutakuwa na dawa ambazo zitatumika kutibu magonjwa yaliyopo.

Alisema: "Unakuta mtu ametoka safari kichwa kinauma kwa uchovu ananunua dawa anameza bila kupata ushauri wa wataalamu lakini mtu anaweza kupewa dozi ya siku tano yeye anatumia siku tatu bila kujali kuwa kuna baadhi ya vimelea vinaweza kuishi na kujenga usugu wa dawa," alisema.



Meneja Mauzo na Usambazaji Magazeti wa Kampuni ya The Guardian Ltd, Dennis Ntaita, akizungumza na mawakala na wauzaji wa magazeti alipokutana nao kwa ajili ya kuweka mikakati ya kufanikisha mauzo ya magazeti ya kampuni hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwenge wa Uhuru kuzindua miradi ya bil.16/-

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MWENGE wa Uhuru unatarajiwa kuzindua miradi 45 ya maendeleo mkoani hapa, yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 16.5.

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Ally Gugu alisema hayo jana wakati akipokea Mwenge huo kutoka kwa Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatma Mganga kwenye makabidhiano yaliyofanyika eneo la Bahi mkoani hapa.

Gugu, alisema Mwenge huo utazindua idadi ya miradi hiyo mkoani hapa kwenye wilaya saba zenye halmashauri nane.

Alisema kati ya miradi hiyo itakayozinduliwa miradi 15 itawekewa jiwe la msingi, miradi 19 itazinduliwa na miradi 11 itatembelewa na Mwenge huo.

Kadhalika alisema Mwenge huo unatarajiwa kukimbizwa kilomita 1,893 kwa maeneo mbalimbali yenye miradi hiyo itakayozinduliwa.

Alitaja miradi hiyo itakayozinduliwa kuwa ni miundombinu ya barabara, majengo ya shule, zahanati, vituo vya afya, madaraja na miradi mbalimbali ya wajasiriamali.

Aidha, alisema mkoa huo umejipanga katika shughuli za maendeleo na utekelezaji wa miradi ya kawaida iliyokusudiwa na serikali inaendelea vizuri.

Alisema serikali ilitoa fedha katika mkoa huo kwa ajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali, wameendelea kuisimamia ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatma Mganga, alisema Mwenge huo ulipokuwa mkoani huko ulizindua miradi 42 ya Sh. bilioni 15.3.

Dk. Mganga alisema katika miradi hiyo mchango wa nguvu za wananchi ni zaidi ya Sh. milioni 46.8 na Mwenge huo ukiwa mkoani Singida walipanda miti zaidi ya 15,000.

Mkuu wa Wilaya Bahi, Godwin Gondwe alisema Mwenge huo ukiwa wilayani kwake utazindua miradi mitano ambayo ni mradi wa kudhibiti taka ngumu katika mji huo.

Gondwe alisema mradi huo utasaidia kusimamia na kuhakikisha taka ngumu zinazozalishwa kutoka kwenye kaya, sehemu za biashara, mashambani, gereji na maeneo ya wazi zinatolewa kwa wakati.

Alisema uzalishaji wa taka katika wilaya kwa siku ni kilo 161,263 sawa na tani 161, uwezo wa kukusanya na kuzoa taka hizi ni kilo 65,000 kwa siku sawa na tani 65.

# Utafiti wa VETA waleta matunda kwa wajasiriamali

**Na Thobias Mwanakatwe,** BAHI

UTAFITI unaofanywa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Kanda ya Kati umeanza kuonesha tija kwa wajasiriamali, kwa kuboresha huduma zao na kujikwamua kiuchumi.

Mkurugenzi wa VETA Kanda ya Kati, John Mwanja, akizungumza juzi wakati wa mafunzo kwa wajasiriamali wanaojishughulisha na upikaji wa vyakula wilayani Bahi mkoani Dodoma, alisema mafunzo wanayoyatoa yameanza kuonesha tija kwa walengwa hasa baada ya kupata mwanga.

"VETA Kanda ya Kati tumekuwa tukifanya utafiti katika maeneo mbalimbali zinapofanyika shughuli za kijasiriamali ili kuona kama zinatija, tunaona sinasifa za kuweza kuwaongezea kipato kikubwa lakini inashindikana kutokana na wahusika kushindwa kujipambanua na kuendelea kufanya ujasiriamali usiowaingizia kipato licha ya maeneo yao ya kazi kuwa na wateja wengi," alisema.

Alisema hadi sasa wameshafanya utafiti tatu ambapo kwa awamu ya kwanza walianza mwaka jana wilayani Ikungi mkoani Singida na baada, walibaini kumekuwa na kuku wengi wa asili ambao wanahitajika kwa kiwango kikubwa katika mikoa mbalimbali ukiwamo wa Dodoma.

Mwanja alisema utafiti wa awamu ya pili waliufanya tena katika wilaya hiyo ya Ikungi baada ya kuzindua Chuo cha VETA na kubaini kuwa kumekuwa na soko kubwa la mbuzi na kondoo wakati wa Sikukuu ya Eid Al Adha ya kuchinja, wanyama hao wamekuwa wakinunuliwa kutoka mikoa mingine kutokana na Singida kutokuwanao wa kutosha.

Alisema kwa awamu ya tatu walifanya utafiti Wilaya ya Bahi na kugundua wilaya hiyo ambayo inamwingiliano mkubwa wa watu, wageni na wasafiri wanaotumia barabara kutoka nchi za jirani kupitia mikoa ya Kanda ya Ziwa kwenda Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam ambao wamekuwa wakipata chakula katika wilaya hiyo.

Alisema VETA Kanda ya Kati ambao wanahudumia mikoa ya Singida, Manyara na Dodoma wamejipanga kuendelea kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali ikiwa ni kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuhakikisha wananchi wanabadilika kiuchumi kwa kujitegemea kutokana na fedha anazozitoa kwa ajili yao.

Hivyo, alitoa wito kwa wananchi wa Wilaya ya Bahi kuwahimiza watoto wao ambao wamemaliza masomo yao ya shule ya msingi, sekondari na vyuo vikuu lakini wapo nyumbani kwenda kujiunga na VETA kilichojengwa wilayani humo kupata stadi za ufundi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Zaina Mlawa, akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo aliwataka washiriki kuzingatia yale ambayo watafundishwa.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo Mwalimu wa Fani ya Upishi VETA Kanda ya Kati Dodoma, Adelina Edward, alisema mafunzo hayo kwa wapishi na watoa huduma ya chakula ni ya muhimu sana na kuwa wameyafanya kufuatia utafiti walioufanya katika wilaya hiyo.

Alisema katika utafiti huo waligundua kuwa watoa huduma wa chakula wa wilaya hiyo katika maeneo kadhaa ya ufanyaji kazi zao wamekuwa na changamoto za namna ya kutunza kumbukumbu, usafi wa chakula, lugha nzuri kwa wateja, uvaaji wenye staha na mambo mengine mengi ambayo yanafanana na hayo ambayo wanapaswa kuyafanya.

Washiriki wa mafunzo hayo, Semeni Athumani, Nicholaus Machimo, Charles Aman na Christina Wilson waliishukuru VETA kwa kuwapelekea mafunzo hayo wakisema yamewaongezea uelewa mkubwa wa utunzaji wa kumbukumbu za mauzo yao jambo ambalo walikuwa hawalifanyi.





# Wasiojulikana wazima mfumo ukusanyaji mapato h'shauri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU chache baada ya watu 40 kukamatwa kwa tuhuma za kubuni na kutumia mfumo feki kuiba mapato ya serikali kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato (POS), serikali mkoani hapa imesema mfumo huo kwa sasa umezimwa na mtu asiyejulikana.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu matumizi ya mfumo na madhara yake ambapo alisema wanaendelea kuwatumia wataalamu kufuatilia mtandao huo.

Alisema awali waliwakamata watu kadhaa akiwemo mbunifu wa mfumo huo ambaye alikuwa anaishi mkoani Dar es Salaam na baadhi ya watumishi wa halmashauri waliokuwa wanashiriki kuuendesha.

Alisema baadhi ya watu hao walifikishwa mahakamani na waliachiwa kwa dhamana isipokuwa wale ambao makosa yao ni ya utakatishaji wa fedha bado wanasota rumande kutokana na makosa hayo kutokuwa na dhamana kwa mujibu wa sheria.

Alisema wameendelea kuwakamata watu mbalimbali ambao walikuwa wanahusika na mfumo huo.

Alisema hivi karibuni kuna watumishi wawili walikamatwa kwenye mikoa ya Songwe na Rukwa wakiwa wanaendelea kukusanya mamilioni ya fedha kwa kutumia mfumo huo.

"Mfano huyu wa Sumbawanga POS yake ilikutwa imekusanya zaidi ya Sh. milioni 300 na huyo wa Tunduma alikuwa amekusanya zaidi ya Sh. milioni 90, wote walisafirishwa na kuletwa Mbeya," alisema Homera.

Alisema waliendelea kufuatilia maeneo ambayo mfumo huo ulikuwa unatumika hasa katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Songwe na Njombe ambayo ndiyo iliyoathirika zaidi na kwamba kwa sasa nchi nzima kunafanyika uhakiki.

Hata hivyo Homera alisema mfumo huo umeshazimwa na wahusika na haifahamiki aliyeuzima ni nani hali ambayo imewafanya waanze kubuni mbinu za kudhibiti mfumo mwingne usifunguliwe na kuleta madhara.

Alisema kwa Mkoa wa Mbeya mfumo huo ulikuwa umeshadhibitiwa na mapato kwenye halmashauri ambazo zilikuwa zimeathirika zaidi yameanza kuongezeka.

Alisema Halmashauri ya Mbarali ambayo ilikuwa ya kwanza kubaini uwepo wa mfumo huo, mapato yake yamepanda na sasa unashika nafasi ya pili kwa mkoa huo ikitanguliwa na Halmashauri ya Chunya ambayo mapato yake yameongezeka kutokana na mauzo ya tumbaku.

Alisema serikali kwa sasa inafuatilia kwa karibu ili kuhakikisha wahuni hao hawabuni mfumo mwingine kama huo na kuutumia kuiba mapato kama ambavyo ilitokea.

Hivi karibuni Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iliwafikisha mahakamani watu 20 kati ya 40 waliobainika kuutumia mfumo huo ambapo kesi hiyo inaendelea kusikilizwa.

# CHAVITA yaiangukia serikali, yaomba wakalimani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), kimeiomba serikali kuajiri wakalimani wa lugha ya alama kwenye taasisi mbalimbali za umma ikiwamo vituo vya kutolea huduma za afya ili kuwasaidia watu wa kundi hilo kupata huduma bora.

Mjumbe wa Bodi ya Utendaji ya CHAVITA Taifa, Subira Upurute, aliyasema hayo juzi kwenye kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Viziwi Duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Mbeya.

Alisema viziwi wamekuwa wakikosa huduma bora za afya kutokana na kukosekana kwa wakalimani wa lugha ya alama kwenye baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya hali ambayo inahatarisha ustawi wa kundi hilo.

"Viziwi wanakosa elimu sahihi ya uzazi na elimu ya kujikinga na magonjwa mbalimbali ikiwamo maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi kutokana na kukosekana kwa wakalimani, tunaomba serikali itusaidia kuboresha mazingira haya mpaka maeneo ya vijijini," alisema Subira.

Alisema yapo baadhi ya maeneo ambayo serikali imefanya vizuri kwa kuboresha mazingira ya viziwi kupata huduma ikiwamo kuanzisha mtaala maalumu wa lugha ya alama kwenye sekta ya elimu hali ambayo inawafanya watu wa kundi hilo kupata huduma vizuri.

Alisema baadhi ya vyombo vya habari vimeajiri wakalimani wa lugha ya alama ikiwamo ITV na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) hali ambayo pia imewarahisishia kupata taarifa.

Alisema wanaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa kushawishi serikali kuboresha mazingira mbalimbali ya upatikanaji wa huduma bora kwa viziwi na watu wengine wenye ulemavu. Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliishauri serikali kuboresha sera na sheria mbalimbali zinazoonekana kuwa kikwazo kwa viziwi kupata huduma na kutekeleza mambo yao.

Alisema endapo mabadiliko hayo yatawasilishwa bungeni atahakikisha yanafanyiwa kazi vizuri kwa maslahi ya kundi hilo pamoja na jamii nzima inayowazunguka.

Aliwaomba Watanzania kuendelea kushirikiana na kundi la viziwi kwenye shughuli mbalimbali za kimaendeleo badala ya kuwatenga kwa maelezo kuwa ni kundi ambalo pia lina uwezo wa kufanya vitu mbalimbali.

"Ni vizuri pia Watanzania tukaendelea kujifunza lugha ya alama ili iwe rahisi kuwasiliana na wenzetu hawa, lakini kwa kuwa Waziri mwenye dhamana ya kundi hili namwomba asaidie kutatua kero mbalimbali za viziwi zikiwemo za kisheria na kisera," alisema Dk. Tulia.

Akifunga maadhimisho hayo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma kwa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

Vilevile alisema serikali inaendelea kusimamia Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010 pamoja na utekelezaji wa sera na matamko ya kimataifa yanayowahusu watu wenye ulemavu mbalimbali wakiwamo viziwi.

Alisema kwa sasa serikali inajenga vyuo vitatu vya watu wenye ulemavu ambavyo vinajengwa katika mikoa ya Songwe, Ruvuma na Kigoma na kwamba tayari serikali imetoa Sh. bilioni sita kwa ajili ya uanza ujenzi huo.

Aliahidi kuwa serikali itaendelea kushirikiana na vyama vya watu wenye ulemavu pamoja na wadau mbalimbali kuratibu shughuli za wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na mikutano ya kujadili kero zinazowakabili.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe, Neema Mwandabila, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kanga wilayani Singwe mwishoni mwa wiki alipokuwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maendeleo. **PICHA:S NEBART MSOKWA**

# Watu 1,000 wenye VVU Njombe hawatumii dawa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU 65,000 mkoani Njombe wamepimwa na kugundulika kuwa na Virusi Vya Ukimwi huku wanaotumia dawa ni 64,000 sawa na asilimia 90.

Hata hivyo kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 Mkoa wa Njombe una watu 800,000.

Hayo yalielezwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Juma Mfanga, wakati wa uzinduzi wa jukwaa la wadau wa ustawi wa watoto mkoani hapa ikiwa ni ishara ya ufunguzi rasmi kwa wadau kuchangia kwa ajili ya watoto.

Akijibu swali walipo watu 1,000, Mfanga alisema mkoa unashughuli nyingi za kibiashara na biashara nyingi za mazao na kuna watu wanaingia na kutoka na wengine watembezi yao binafsi kwa hiyo kwenye taratibu za kutoa huduma wanatakiwa wafahamu wale wanaopewa huduma.

Alisema mwaka jana katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika mkoani Lindi Rais Samia alitoa maekekezo mahususi kwamba lazima tushughulike na kundi la vijana na watoto.

"Ndani ya mkoa wetu tunachangamoto hiyo hata sisi na sehemu kubwa ya maambukizi yapo kwenye kundi hilo la vijana"alisema Mfanga.

Alisema kwa watoto chini ya miaka mitano ambao wamewatambuliwa katika mradi huo wapo watoto 25,000 ambao wanaishi katika mazingira hatarishi na kati yao watoto takribani 4,000 ndio wanachangamoto ya VVU.

Mkurugenzi wa Mradi wa Kizazi Hodari, Dorothy Matoyo, alisema mradi huo unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), kupitia mfuko maalum wa dharura wa kupambana na UKIMWI wa Rais wa Marekani (PEPFAR), na unatekekelezwa na Deloitte kwa kushirikiana na Tanzania, kupitia Wizara ya Mandeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ili kuhakikisha mapambano dhidi ya VVU yanafanikiwa.

Dorothy alisema mradi huo umefanikiwa kugharamia bima kwa kipindi cha kuanzia Septemba 2023 hadi Septemba 2024 zenye thamani Sh. milioni 38 ambayo ni malipo ya bima ya afya ya jamii kwa kaya 1,279 zenye watoto 2,128 mkoani Njombe.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema kuwa udumavu ni hatari kwa taifa hivyo hakutakuwa na usalama kwa taifa kama nusu ya taifa litakuwa limedumaa.



## Waomba kufundishwa elimu ya uzazi wajikinge na wahuni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Jendele Mkoa wa Kusini Unguja wamesema wakati umefika kwa wanafunzi wenye umri zaidi ya miaka 14 kupewa elimu ya afya ya uzazi na stadi za maisha, ili kujikinga na makundi hatarishi.

Waliyasema hayo baada ya kumaliza kupewa mafunzo ya afya uzazi na stadi ya maisha yaliyotolewa na mradi wa kuongeza mazingira rafiki ya kujifunzia maisha na Taasisi ya Korea Food for the Hungary International chini ya ufadhili wa Shirika la KOICA yaliofanyika katika Shule ya Jendele.

Walisema elimu hiyo ni muhimu kwa sababu vijana wengi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali na kushindwa kuhimili mihemko na kujiingiza katika vikundi viovu.

Rajab Ali Rajam ni miongoni mwa wanafunzi wa shule hiyo, akizungumza kwa niaba ya wenzake alisema wasichana na wavulana wanapofikia umri wa kubalehe wanahitaji washauri wazuri wa kuwapa nasaha ili kutoshiriki vitendo vya ngono.

Alisema wengi wao wanajiingiza katika vitendo viovu ikiwamo ngono, matumizi ya dawa za kulevya kutokana na kukosa elimu ya kujitambua na stadi ya maisha.

“Wasichana na wavulana wanapobalehe huwa na mabadiliko katika miiili yao na kuwa na mihemko na matamanio ambapo ukishindwa kujidhibiti unaingia katika kufanya vitendo viovu ambavyo husababisha kupata mimba za umri mdogo, HIV na maradhi mbalimbali ya kuambukiza,” alisema mwafunzi huyo.

Aidha, aliipongeza Taasisi ya KFHI kwa kuwapa elimu hiyo akisema imewasaidia kujitambua na kuahidi kuwa mabalozi wazuri kwa wasichana na wavulana wezao ili kuepukana na vishawishi ambavyo vitahatarisha afya zao.

Mwanafunzi mwingine Mwanahamu Said alisema wasichana ndio waathirika wakubwa wa vitendo vya udhalilishaji kutokana na mabadiliko mbalimbali hasa ya sayansi na teknoloji, hivyo elimu ya kujitambua na afya ya uzazi inahitajika kwao.

Mwalimu wa shule hiyo, Fatma Haji alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo wanafunzi wao kwa vile wengi wao wapo katika umri wa hatari ambao wanakumbana na changamoto nyingi ikiwemo vishawishi na mabadiliko ya mwili.

“Kawaida wanafunzi wanapofika umri wa miaka 14 huwa wapo katika hatari na ni umri ambao hukumbana na viashiria vingi na kutaka kujaribu bila ya kujua athari ya kile wanachotaka kujaribu, hivyo mafunzo hayo ni muhimu,” alisema.

Aidha, alisema hivi sasa lazima jamii ishirikiane katika malezi ya pamoja kwasababu kunachangamoto nyingi zinazowakumba vijana ikiwamo utumiaji wa dawa za kulevya, mimba za umri mdogo.

Akifunga mafunzo hayo, mmoja wa wahusika wa mradi kutoka Taasisi ya KFHI, Esther Mwakalobo, alisema awali mafunzo hayo waliyatoa kwa walimu wa shule hiyo ili kuwafundisha wanafunzi elimu ya kujitambua na kufahamu masuala ya afya ya uzazi.

Alisema kupitia mradi huo shule tano zilizomo katika mradi zitafikiwa, kupewa elimu ambazo ni Jendele, Fukuchani, Mtule, Chwaka Tumbe na Shumba Viamboni.

# RC apiga marufuku uvunaji, usafirishaji embe changa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amepiga marufuku uvunaji na usafirishaji wa embe ambazo hazijakomaa katika mkoa wake.

Alitoa tamko hilo wakati akijibu maswali ya wananchi wa Donge mkoani Kaskazini Unguja wakati wa mkutano wa kusikiliza kero za wananchi.

Pamoja na mambo mengine wananchi hao walilalamika changamoto ya uvunaji na usafirishaji wa embe hizo na kupelekwa sokoni kwa ajili ya biashara.

Ayoub alisema zipo embe maalum ambazo zinakubalika kuvunwa zikiwa changa kwa sababu ya mahitaji mbalimbali na kupelekwa sokoni, lakini siyo kwa kila embe hivyo ni vyema wasafirishaji wa mazao kufuata utaratibu wa kukata vibali vya kusafirisha mazao.

“Zipo embe ambazo zinajulikana hizi ni kwa ajili ya kiungo kama kuweka katika mchuzi embe hizi zinaruhusiwa kuvunwa zikiwa changa lakini embe za kabila mfano borimo au dodo ni marufuku kuvunwa zikiwa change,” alisema Ayoub.

Awali wananchi wa kijiji hicho, walisema kuna uharibifu mkubwa wa uvunaji wa embe ambazo hazijakomaa na kusafirishwa kupelekwa sokoni kwa ajili ya kuuza jambo ambalo linarejesha nyuma juhudi za wakulima.

Juma Makame, alisema uvunaji huo ni hujuma katika kilimo na kutasababisha Zanzibar kuwa na upungufu wa embe na kutegemea kutoka nje ya kisiwa hicho.

Ofisa Kilimo wa Mkoa huo, Juma Khamis Kona, aliwataka masheha wa shehia kusimamia suala la vibali vya usafirishaji wa mazao ili kuhakikisha mazao yanayosafirishwa yamekomaa na yanastahili kuvunwa.



Baadhi ya wazee wakifuatilia hotuba katika maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani katika ukumbi wa mikutano wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mashindano ya Tigo/Zanteli kukuza utalii wa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MASHINDANO ya mbio za kimataifa za Tigo/Zanteli yanatarajia kufanyika Oktoba 29 mwaka huu, kuwakutanisha wageni kutoka mataifa mbalimbali kwamba yatasaidia kukuza sekta ya utalii visiwani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Kanda Tigo/Zantel upande wa Zanzibar, Azizi Saidi Ali, alisema mbio hizo zitakuwa za kilomita tano, 10 na 21, zitasaidia kuibua vipaji, kukuza uchumi na kuimarisha afya za wananchi. “Wakimbiaji wote wa zenji kwa spidi ya 5G, kwenye visiwa vya Karafuu kwa ajili ya Tigo/Zantel Zanzibar International Marathon,” alisema.

Alisema, dhamira ya mbio hizo ni kuendelea kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii kwa kuwekeza kwenye miradi yanayogusa hisia za maisha ya wateja wao kupitia mbio hizo.

Azizi aliwataka wananchi hasa vijana kuendelea kujisajili na usajili unafanyika kidijitali, hivyo wateja wa tigo wapige *150*01# kwa ajili ya kushiriki ili kujitangaza katika mataifa mbalimbali.

Wakizungumza kuhusu mbio hizo wadau wa utalii na michezo, walisema mbio hizo ni fursa nzuri ya kuitangaza Zanzibar kiutalii na kimichezo ambapo sekta ya utalii ni sekta mama katika kukuza uchumi wa visiwa hivyo. Mmoja ya wadau hao, Rashid Mohamed Rashid, alisema, sekta ya utalii kwa Zanzibar ina uwanja mpana hasa ukizingatia kuwa eneo hilo ni la uchumi wa buluu ambao ndio mkakati wa serikali.

Alisema, jambo hilo siku zote limekuwa linaratibiwa vizuri na huwakutanisha watu kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania na nje ya nchi.

Naye Omar Amir Suleiman, alisema ni vyema waandaaji wa mbio hizo kuendelea kuitangaza zaidi Zanzibar na kuwahamasisha wananchi kushiriki mashindano hayo ili kuchangia sehemu kubwa ya ushiriki kupitia tamasha hilo.

Aidha alisema utalii wa kichocheo cha mapato ya nchi na huchangia kuboresha uchumi sambamba kusaidia kuongeza kipato kupitia sekta ya michezo.

# Wanafunzi waliokosa vyuo vikuu waonyeshwa fursa

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Elimu ya Vyuo Vikuu Nje ya Nchi, Global Education Link (GEL), imewataka wazazi wenye watoto waliokosa nafasi za kusoma vyuo vikuu ndani ya nchi wasipate mfadhaiko wa moyo na badala yake waombe vyuo vya nje ambavyo vinatoa nafasi za fani mbalimbali.

GEL imesema nafasi nje ya nchi bado ni za kutosha na inatarajia kusafirisha zaidi ya wanafunzi 1,500 kwa mwaka huu wa masomo kwenda kusoma nchi mbalimbali duniani zikiwamo China, India, Cyprus, Uturuki, Hungary kwa uchache.

Mkurugenzi wa GEL, Abdlulmalik Mollel, alisema hayo wakati akizungumza na wazazi na wanafunzi zaidi ya 100 ambao walisafiri mwishoni mwa wiki kwenda nje ya nchi kuanza mwaka wa masomo.

Alisema wanafunzi hao walielezwa mambo ya msingi ya kuzingatia kabla ya safari, wakati wa safari na baada ya kufika kwenye nchi wanazokwenda hasa kuzingatia masomo na kuachana na biashara zingine ambazo zitawapotezea malengo.

Alisema anafahamu wanafunzi wengi wanaotaka kusomea fani za uhandisi na udaktari wamekosa nafasi kutokana na ushindani mkubwa kwenye vyuo vya ndani, lakini hawana sababu ya kupata msongo wa mawazo kwa kuwa nafasi zipo kwenye vyuo mbalimbali nje ya nchi.

"Tunafahamu kwamba wanafunzi wengi hasa wa masomo ya uhandisi na fani za afya kama udaktari wamekosa kwasababu nafasi zilikuwa chache kwa hapa nchini, lakini njooni ofisi za Global Education Link tutahakikisha watoto wenu wanapata nafasi ndani ya muda mfupi uliobaki na watasafiri kwenda kusoma vyuo mbali mbali nje ya nchi," alisema.

Mollel alisema, wanafunzi watakaopata changamoto ya ada watapatiwa mikopo isiyo na riba kwa ajili ya ada ili wawahi mwaka wa masomo.

"Wazazi mliobahatika kuja hapa leo tunaomba muwatangazie wazazi wengine ambao watoto wao wamekosa nafasi za vyuo vikuu Tanzania kwamba ndoto za watoto wao zinaweza kutimia kwa kuwa nafasi zipo, waje kwetu tutawapa Visa na tiketi ndani ya muda mfupi, wasikae kinyonge wakadhani watoto wao wamekwama kabisa," alisema.

"Wazazi lazima watambue kwamba mtoto wako anaweza kuwa amepata daraja la kwanza, lakini anazidiwa na wenzake waliochukuliwa kwenye vyuo vya hapa nchini, lakini hiyo haimaanishi kwamba amefeli, amekosa nafasi kutokana na ushindani uliokuwapo kwa hiyo njooni GEL tuwaunganishe na vyuo vya nje ya nchi nafasi bado zipo wataenda kusoma," alisema Mollel.

Alisema wanafunzi wa vyuo vikuu ni watu wazima wanaotakiwa kuanza kutatua changamoto watakazokutana nazo kwa kuwasiliana na maofisa wa vyuo vikuu vilivyopo au maofisa wa Global na kuachana na kasumba ya kuwasumbua wazazi wao kwa kila jambo watakaloona haliko sawa.

"Unakuta mwanafunzi kaona mende chumbani kwake anapiga picha anamrushia mzazi wake sasa unataka mzazi wako asafiri kuja China kuondoa mende? Ukiwa mwanafunzi wa chuo kikuu ni mtu mzima unayeweza kukabiliana na changamoto kwa hiyo siyo kila kitu unamwambia mzazi wako. Kama umekuta chumba ni kichafu safisha, kama umekuta mende muondoe siyo unamwambia mzazi wako," alisema Mollel.

"Udahili wa vyuo vikuu vya ndani umefikia ukingoni, dirisha la pili limefungwa dirisha la tatu nalo linatarajiwa kufungwa inawezekana kukawa na kundi kubwa linataka kusomea udaktari wa meno, moyo, mama cheza, famasia, uhandisi na zinginezo sasa kama kuna mwanafunzi amekosa kozi ya yoyote ya sayansi, asihisi amechelewa aje Global atapata nafasi nje ya nchi," alisema.




Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Bristow, akiwakabidhi mfano wa hundi ya dola za kimarekani elfu 10 wakurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Asia Halamga Foundation, Nuru Bondi (kulia) na Farida Joel (kushoto), kwa ajili ya kusaidia shirika hiyo kuhudumia watoto wenye mahitaji maalum katika hafla iliyofanyika Mgodi wa North Mara mkoani Mara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bodaboda afariki dunia kwa kugongana na lori

**Na Samson Chacha,** TARIME

DEREVA wa bodaboda, Samwel Zakaria, maarufu Mkulima, amefariki dunia baada ya kugongana uso kwa uso na lori aina ya Scania lenye namba za Usajili KBX 188Z.

Wakizungumzia tukio hilo, Diwani wa Kata ya Sirari, Amos Sagara na Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Wakuru Mirumbe, walisema ajali hiyo ilitokea Alhamisi katika Kijiji cha Buriba, Kata ya Sirari wakati Zakaria akienda mjini Tarime akiwa amebeba mifuko ya saruji.

Viongozi hao walisema dereva huyo wa bodaboda aliyekuwa kwenye mwendokasi alipofika Kijiji cha Buriba ambako kuna mteremko na kona, alikumbana na lori la mizigo lililokuwa limetoka mizani umbali wa mita 100 na inadaiwa aliyumba na kukosa mwelekeo na kwenda kuligonga lori hilo uso kwa uso na kusababisha kifo chake papo hapo.

"Tunawaasa vijana waendesha bodaboda kufuata sheria za usalama barabarani na vilevile kufanya biashara halali kwa kulipia ushuru na kodi badala ya kufukuzana na watumishi wa Idara ya Forodha hali inayochangia ajali kama hizo," alisema mmoja wa viongozi hao.

Alisema vijana wanaosomba bidhaa ndogo toka nchi jirani ya Kenya kupitia njia za panya, wanaendesha pikipiki zao kwa mwendo kasi bila kuchukua tahadhari na kusababisha ajali za mara kwa mara.

Polisi Kituo cha Sirari, imethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema wanamhoji dereva wa lori hilo kwa uchunguzi zaidi na kuonya waendesha bodaboda kufuata sheria za usalama barabarani na kufanya biashara halali.

# Mwalimu Sekondari Wasichana Jokate mfano wa kuigwa

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

MKUU wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Jokate Mwegelo iliyopo Wilaya ya Kisarawe, Mariam Mpunga, amesema ili kuwa na wasichana wengi wanasayansi, madaktari na wahandisi kutoka shule hiyo amekuwa na utaratibu wa kuwatumia wahadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutoa ushuhuda.

Vilevile, huwaleta madaktari wa kike na wataalamu wa sayansi kutoka sehemu mbalimbali kuzungumza na wasichana wa shule hiyo na kuwapa ushauri kuhusu kusoma masomo ya sayansi na faida zake kwa baadaye.

Mpunga, alisema ameamua kubuni utaratibu huo ili kuokoa wanafunzi wa kike wanaochaguliwa kusoma masomo ya sayansi na baadaye kubadilisha tahsusi wakihofia ugumu wa kusoma masomo hayo.

Aliyaeleza hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na Nipashe ofisini kwake baada ya kuhitimisha hafla ya kuwakaribisha wanafunzi wa kidato cha tano waliochaguliwa kujiunga na shule hiyo.

Alisema, kwa kuwa shule hiyo ni ya mkondo wa sayansi na malengo yake ni kutokomeza daraja la tatu, amelazimika kubuni mbinu hiyo kuwawezesha wanafunzi wanaosoma shule hiyo kutoogopa masomo hayo na kutumia muda mwingi kujisomea na kuwa na ufaulu wa juu.

Kadhalika, alisema ili kuwa na idadi kubwa ya wanasayansi hususani wa kike, serikali inatakiwa kuwa na utaratibu wa kuwaandaa watoto hao kusoma masomo ya sayansi wakiwa shule za msingi kabla ya kufika sekondari.

Pia aliomba wadau mbalimbali kusaidia ujenzi wa uzio katika shule hiyo ili kuimarisha ulinzi kwa watoto hao wa kike na kuiomba jamii kutoa ushirikiano katika mambo mbalimbali ikiwamo la ulinzi.

Alisema kwasasa shule hiyo ina upungufu wa maabara na vifaa na kuomba wadau kusaidia kulitatua ili kuondoa kikwazo kwa wanafunzi wanao hitaji kusoma kwa vitendo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Mohamed Boniface, aliwasihi walimu kuwa na maadili mazuri wawapo shuleni kwa kuwa wao ndio kielelezo kwa wanafunzi.

Alimtaka Ofisa Elimu Sekondari wa wilaya hiyo kuandaa barua ya kumpongeza mwalimu huyo kwa kazi anazozifanya na kwa kusimamia kwa kasi miradi inayoletwa katika shule hiyo.

Ofisa Elimu Takwimu wa wilaya hiyo, Hassan Mathias, aliwasisitiza wanafunzi kusoma kwa bidii na vikwazo vilivyopo visiwe sababu ya wao kufeli kwa kuwa serikali inaendelea kuvishughulikia.

# Waziri apongeza kozi mpya usafirishaji NIT

**Na Prosper Makene**

NAIBU Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, amepongeza Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kwa kuanzisha kozi mpya zitakazosaidia serikali kwenye sekta ya usafirishaji.

Katika ziara yake ya kwanza katika chuo hicho kilichoko Mabibo, Dar es Salaam, Naibu Waziri huyo aliwaambia waandishi wa habari kuwa sasa serikali inawekeza fedha nyingi katika miradi ya usafirishaji ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), bomba la mafuta na miradi mingine mingi katika sekta ya usafirishaji, hivyo NIT haina budi kuendelea kuongeza kozi ambazo zinalenga kutoa wafanyakazi ambao watafanya kazi katika miradi mikubwa ya serikali.

"Miongoni mwa watu waliomwelewa vyema Rais Samia ni Prof. Zacharia Mganilwa (Mkuu wa NIT), ameanzisha miradi mbalimbali ya kimkakati ambayo ina uwezo wa kuzalisha rasilimali watu ya kutosha kukidhi mahitaji ya sekta ya usafiri na usafirishaji.

"Prof. Mganilwa pia amekuja na miradi mikubwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa chuo cha reli NIT Tabora pamoja na kujenga kampasi nyingine ya NIT mkoani Lindi," alisema.

Kihenzile alipongeza taasisi hiyo kwa kuanzisha kozi za usafiri wa anga ikiwa ni pamoja na kuwa na vifaa vya kisasa na karakana za kisasa kwa ajili ya mafunzo ya anga.

"Badala ya kupeleka ndege zetu Ulaya kwa ajili ya matengenezo, sasa ndege nyingi zitakuwa zinafanyiwa ukarabati na watalaamu wanaozalishwa katika chuo hiki," alipongeza.

Naibu Waziri huyo pia aliziagiza kampuni za CRJE (East Africa) Limited na Nandhra Engineering and Construction Company Limited zinazojenga majengo matano katika kampasi kuu ya NIT Mabibo ikiwa ni sehemu ya msaada wa Benki ya Dunia (WB), kukamilisha kazi za ujenzi huo kwa muda ulipangwa katika mikataba.

Kampuni ya Nandhra Engineering and Construction Company Limited ilimhakikishia Naibu Waziri kuwa itakamilisha mradi huo kwa wakati, lakini Kampuni ya CRJE (East Africa) Limited ilisema kuwa ujenzi wa majengo wanayojenga hautamaliza mwezi Novemba mwaka huu kama walivyopanga kutokana na sababu mbalimbali ambazo zilikuwa nje ya uwezo wao. Watakabidhi majengo hayo ifikapo Machi mwakani.

Katika ziara hiyo Naibu Waziri pia alielekeza NIT kuanzisha vituo vingi vya ukaguzi wa magari nchini ili kuongeza ufanisi katika ukaguzi wa magari.

Alisema ni jambo zuri kwa chuo hicho kuanzisha kituo cha ukaguzi wa magari kwa kuwa idadi ya magari yaliyomo nchini ni zaidi ya milioni 2.5 huku Dar es Salaam ikiwa na nusu ya magari hayo.

Alitoa wito kwa taasisi za umma na binafsi kufanya ukaguzi wa magari yao ili kupunguza ajali za barabarani.

Alisema ni wakati wa kutumia miundombinu hiyo kukagua magari kabla ya kuanza kutumika ili yawe na ubora.

"Ninaelekeza mamlaka zinazosimamia vyombo vya usafiri kuhakikisha zinakaza nati kwa lengo la kunusuru maisha ya watu wasio na hatia na nguvu kazi ya taifa," aliagiza Kihenzile.

Pia alielekeza NIT waongeze hosteli nyingi ili kuchukua wanafunzi wengi na kupunguza changamoto ya wanafunzi kupanga nje ya shule ambako hakuna mazingira rafiki.

Alisema idadi ya wanafunzi inaongezeka, sasa wamefikia 15,000 na wanatarajiwa kupokea wanafunzi wengi zaidi.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Mganilwa, alisema kituo cha ukaguzi wa magari kilijengwa kwa ajili ya wanafunzi wao, maofisa wa polisi wanaohusika na ukaguzi na maofisa wa bima.

Alisema wanachokifanya maofisa wa bima ni kuangalia thamani ya gari baada ya kupata ajali na kisha kuwalipa wateja wao.

"Tumekuwa tukihamasisha umma walete magari yao ili kujua ubora wake kwa kuwa tunakagua zaidi ya mifumo 15 hasa inayoendana na usalama wa gari,'' alifafanua.

Prof. Mganilwa pia alisema watu wanaouziana magari pia wana wajibu wa kupeleka magari hayo kufanyiwa ukaguzi kabla ya kununua ili yakaguliwe na watapewa taarifa ya gari husika.

"Baada ya ukaguzi tutatoa ripoti ambayo huenda mnunuzi badala ya kununua kwa Sh. milioni nane anaweza kuambiwa gari linahitaji matengenezo ya Sh. milioni 12, hivyo akajikuta ananunua gari kwa Sh. milioni 20," alifafanua.

Alisisitiza kuwa wanahamasisha Watanzania watumie kituo hicho kwa kuwa ukaguzi wa gari dogo huanzia Sh. 60,000 huku gharama ya magari makubwa hutegemea na mahitaji na kwamba kituo hicho kitawasaidia kuwa na uhakika wa kupunguza ajali za barabarani.




Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya Exim Tanzania, Shan Kinswaga (wa pili kulia) na Kamishna wa Polisi, Liberati Sabas Materu (katikati), wakitia saini Mkataba wa Makubaliano (MoU) jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa benki hiyo, Edmund Masaga, Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa Jeshi la Polisi, ASP Ezekiel Midala (kushoto) na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, (SACP) Gustavus Babile (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jeshi la Polisi laingia makubaliano mikopo maalum kwa askari wake

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi limeingia Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Benki ya Exim unaolenga kuwezesha utoaji mikopo ya masharti nafuu kwa askari polisi kupitia programu maalum ya benki hiyo ijulikanayo kama 'Wafanyakazi Loan'.

Makubaliano hayo mapya yaliyotiwa saini jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, yanalenga kutekeleza azma ya benki hiyo kuendelea kuwawezesha Watanzania kifedha kupitia utoaji huduma za kibenki na kuongeza ushirikishwaji wa kifedha nchini.

Akizungumza kabla ya utiaji saini huo, Kamishna wa Polisi, Fedha na Lojistiki, Liberati Materu aliyemwakilisha Mkuu wa Jeshi hilo, IGP Camilius Wambura, alisema makubaliano hayo yamekuja wakati mwafaka na kuishukuru benki hiyo kwa imani yake kwa jeshi.

"Wachumi wanaamini kuwa huwezi kufanya maendeleo bila kukopa, lakini hili linahitaji nidhamu kubwa. Ninaishukuru Benki ya Exim kwa kuendelea kuwa na imani na taasisi yetu na kuridhia kutoa mikopo kwa maofisa wetu wa polisi. Ninaamini mikopo hii itasaidia kuboresha ustawi wao wa kijamii na kiuchumi iwapo itatumika ipasavyo," alisema Kamishna Materu.

Alisisitiza dhamira ya Jeshi la Polisi kuendelea kufanya kazi kwa karibu na benki hiyo ili kuhakikisha mpango huo wa 'Wafanyakazi Loan' unakuwa na tija kwa askari wa jeshi hilo.

"Kama taasisi, tuna mifumo thabiti na tutahakikisha makubaliano haya yanatelezwa kwa ukamilifu. Yeyote atakayeweza kupata mkopo kupitia programu hii atakuwa na wajibu wa kulipa kama ilivyokubaliwa hapo awali," alisisitiza.

Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya Exim, Shani Kinswaga, alisema mkataba huo mpya uliotiwa saini kati ya benki yake na Jeshi la Polisi, pamoja na mambo mengine, utasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha uhusiano baina ya taasisi hizo mbili.

Shani alisema benki hiyo itaendelea kuwa mstari wa mbele kusaidia kukuza sekta ya kifedha kwa kutoa huduma za kifedha bila vikwazo, huku ikitumia suluhu za kidijitali na huduma zinazotengenezwa mahususi.

"Tumefanya vikao na Jeshi la Polisi kuhusu jinsi tunavyoweza kutekeleza azma yetu ya kutoa mikopo kwa askari wa Jeshi la Polisi kwa kuhakikisha pande zote mbili zinanufaika.

"Tunayo furaha leo kwa kuwa majadiliano yetu yametimia kwa kusaini mkataba huu. Kama benki, tunashukuru kwa fursa hii ya kipekee na imani tuliyopewa na tunaamini mikopo itakayotolewa kupitia programu yetu ya 'Wafanyakazi Loan' itakuwa chachu ya maendeleo," Shani alisema.

Alibainisha kuwa kupitia programu hiyo maalum, askari polisi watakopa kuanzia Sh. milioni moja hadi Sh. milioni 160 na kuzirejeshwa kati ya miezi sita hadi 96 kutegemeana na ahadi ya mkopaji ambayo inaweza kutumika kutekeleza ndoto za mkopaji ikiwa ni pamoja kupata mkopo wa nyumba, kununua magari na kulipia ada ya masomo ili kujiendeleza kielimu.

"Tofauti na mikopo mingine iliyopo sokoni kwa sasa, wakopaji kupitia programu yetu ya 'Wafanyakazi Loan' hawalazimika kutoa dhamana yoyote kama sharti.

"Mkopaji anahitaji tu kuwa na hati ya mishahara, taarifa ya benki na barua ya utambulisho kutoka kwa mwajiri wake na baada ya kukidhi mahitaji hayo machache, mkopaji atapokea mkopo yake ndani saa 48 tu," alifafanua.

Shani alitoa angalizo kwa wakopaji kupitia programu hiyo kutumia fedha zilizokopwa kwa busara kutekeleza miradi ambayo itaongeza thamani huku akiwasihi kuandaa mpango maalum wa marejesho ili kuhakikisha mikopo hiyo inalipwa kwa wakati.

"Benki ya Exim tuna shauku ya kutengeneza fursa kwa wateja wetu. Ni matumaini yangu kuwa endapo mikopo hii itatumika vyema, basi itasaidia kutoa suluhu mbadala za kifedha kwa maofisa wa polisi ili kutimiza ndoto zao," alisema.

## HABARI MICHEZO

# NBC, NYOTA AZAM, TWIGA STARS WAENDESHA KLINIKI YA MICHEZO

**Na Mwandishi Wetu**

MDHAMINI Mkuu wa Ligi ya Kuu ya Tanzania Bara, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), imeendesha programu yake ya michezo kwa watoto inayofahamika kama 'NBC Chanua Account Football Clinic' ikilenga kuibua vipaji vya watoto wadogo.

**Hatua hiyo ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo katika kukuza mchezo wa soka hapa nchini.**

Katika kufanikisha programu hiyo iliyofanyika viwanja vya Agha Khan, eneo la Mawasiliano jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, benki hiyo ilihusisha wadau mbalimbali wakiwamo wazazi na watoto wao walioungana na baadhi ya wachezaji vinara kutoka klabu ya soka ya Azam FC wakiwamo Prince Dube, Abdul Suleiman 'Sopu', Lusajo Mwaikenda na Iddi Selemani Nado.

Pia walikuwapo baadhi ya wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake, Twiga Stars, Stumai Abdallah na Fatuma Issa. Kupitia programu hiyo benki hiyo pia ilikabidhi mipira 30 kwa Academy ya Vijana ya Magnet ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za taasisi hiyo kulea na kuendeleza vipaji vya michezo hapa nchini.

Akizungumzia programu hiyo, Meneja Masoko wa NBC, Alina Kimaryo, alisema ni mwendelezo wa jitihada za benki hiyo kukuza mchezo huo sambamba na kuchochea kasi ya ajira nchini kupitia sekta ya michezo.

"Mkakati wa NBC kwa sasa ni kuhakikisha sekta ya michezo inageuka kuwa ajira. Katika kufanikisha hili tulianza na udhamini wa Ligi Kuu ya NBC, tukaona pekee haitoshi, tukaongeza udhamini wetu hadi kwenye Ligi ya Championship na sasa kupitia programu yetu hii ya NBC Chanua Account Football Clinic, tunalenga kuibua vipaji chipukizi kabisa vya mchezo huu pendwa.

"Katika kufanikisha hili pamoja na kuandaa programu za mazoezi kwa watoto, tutakuwa pia tunawakutanisha na wachezaji vinara hapa nchini ili waweze kuwapa hamasa chipukizi hawa waongeze juhudi kwenye michezo huku pia wakiwapa mbinu mbalimbali za kimichezo," alifafanua.

Kwa mujibu wa Alina, kupitia programu hiyo inayotarajiwa kufanyika angalau mara nne kwa mwaka, walengwa ambao ni watoto wenye umri kuanzia miaka sita hadi 13, watapata fursa ya kupewa elimu kuhusu fedha hususan umuhimu wa kujiwekea akiba huku wazazi pia wakipata nafasi ya kupewa elimu kuhusu malezi ya watoto hasa kwenye masuala yanayohusiana na ulaji wa vyakula sahihi, umuhimu wa mazoezi, mabadiliko ya ukiukaji kwa watoto na namna ya kutambua vipaji vya watoto wao.

Wakizungumzia hatua hiyo wachezaji walioshiriki programu hiyo, pamoja na kuipongeza NBC kwa jitihada zake katika kuendeleza mchezo wa soka hapa nchini, walionesha kufurahishwa zaidi na mpango huo kwa kuwa unatoa fursa kwao kushirikiana na jamii hususan watoto, hatua ambayo itasaidia sana kuwashawishi wazidi kuupenda mchezo huo sambamba na kuongeza juhudi zaidi waweze kufanikisha ndoto zao kupitia michezo.

"Imekuwa ni furaha sana kwetu hii leo na kwa hili tunawapongeza sana NBC kwa kuwa kupitia program hii ya NBC Chanua Account Football Clinic wametukutanisha na watoto ambao tumeweza kucheza nao, tumewaelekeza baadhi ya mbinu chache za kimichezo na zaidi tumewahamasisha waendelee kupenda michezo sambamba na kuzingatia masomo yao kwa kuwa elimu na michezo vinakwenda sambamba," alisema kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Sopu.



Baadhi ya wachezaji watoto na wazazi, wakimfuatilia mchezaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Stumai Abdallah, wakati akielekeza mbinu mbalimbali za mchezo wa mpira wa miguu kwa watoto hao walioshiriki programu mpya ya michezo kwa watoto inayofahamika kama NBC Chanua Account Football Clinic, inayoratibiwa na Benki ya NBC, inayolenga kuibua vipaji vya watoto wadogo. Programu hiyo ilifanyika viwanja vya Aghakhan, eneo la Mawasiliano jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

## Kundemba yatoa sababu vichapo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kundemba FC imesema kupoteza michezo miwili mfululizo kwenye Ligi Kuu Zanzibar kumetokana na kuwapo kwa wachezaji majeruhi ambao wanatoka kikosi cha kwanza.

Kundemba FC juzi ilikubali tena kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Maafande wa KVZ mchezo uliochezwa katika Dimba la Mau A majira ya saa kumi alasiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Vuai, alisema bado ana wachezaji majeruhi watano ambao ni tegemeo katika kikosi chake wakiwa tayari wamekosa michezo yote miwili waliyopoteza.

Alisema kutokana na ligi hiyo kuwa ngumu katika mzunguko huu wa awali, ukikosa wachezaji hata wawili tegemeo ni ngumu kupata matokeo mazuri hasa ya alama tatu.

## Stand Utd moto Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Stand United juzi ilipata ushindi wa pili mfululizo katika Ligi ya Championship inayoendelea, baada ya kuichakaza Copco kutoka Mwanza mabao 2-1, mechi ikipigwa Uwanja wa Kambarage Shinyanga huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zulfikir Mahdi, akitamba kuwa gari sasa ndiyo limewaka.

Stand United ilishinda mechi yao ya kwanza wiki iliyopita kwa bao 1-0 kwenye uwanja huo huo dhidi ya Pamba pia ya Mwanza kwa bao pekee la Emmanuel Mtambuka.

Alikuwa ni Halifa Nolo aliyepachika mabao yote mawili, la kwanza likifungwa dakika ya 44 kwa mkwaju wa penalti, huku akipachika lingine dakika ya 67.

"Niliwaambia mashabiki wa Stand United waje uwanjani wasiwe na wasiwasi kwa sasa gari limewaka, tulishinda mechi iliyopita na sasa tumeendeleza, na mechi ijayo sasa tunakwenda kucheza ugenini dhidi ya Biashara United, nawaomba mashabiki watakaoweza kwenda waje kutusapoti na wale ambao watabaki nyumbani watuombee," alisema Kocha Mkuu wa Stand United, Mahdi.

# TPBRC yawapa kina Mwakinyo, Paf Sports siku saba

**Na Shufaa Lyimo**

KAMISHENI ya Ngumi za Kulipwa nchini (TPBRC), imetoa siku saba kwa Paf Sports Promotion pamoja na Hassan Mwakinyo, kupeleka vielelezo vyao vinavyoonesha kwa nini pambano lililokuwa lifanyike Ijumaa halikufanyika kama ilivyopangwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Kamisheni hiyo, George Silas, alisema baada ya siku hizo watatoa taarifa rasmi kwa Watanzania wajue kile kinachoendelea.

"Tumetoa siku saba kwa Mwakinyo na Karigo walete vielelezo vyao kwa nini pambano halikuweza kufanyika, tujue nini kinaendelea kati yao, hatujui kilichosababisha Mwakinyo agome kupigana baada ya hapo tutatoa tamko rasmi kwa Watanzania na wadau wa ngumi wajue kinachoendelea," alisema Silas.

Alisema wanalaani kitendo hicho kwani kinachafua mchezo wa ngumi Tanzania na kwamba hawatakubali kufanya kazi na bondia au promota mwenye lengo la kuuchafua mchezo huo.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Chama cha Mabondia Tanzania, Japhet Kaseba, amewataka mabondia wajiunge na chama chao ili kama wakipata matatizo wapate urahisi wa kusaidiwa.

"Ninaomba kila bondia ajiunge na chama ili kama atapata changamoto yoyote anapata urahisi wa kusaidiwa," alisema Kaseba ambaye aliahidi kukaa na kuzungumza na pande zote mbili na kamisheni hiyo itatoa taarifa rasmi ya nani waliyemchukulia hatua. Naye Mwenyekiti wa Chama cha Mapromota Tanzania, Evarest Mopao, amewaomba radhi Watanzania kwa kile kilichotokea siku hiyo.

"Tunalaani vikali kitendo kilichofanywa na Hassan Mwakinyo, kwani Watanzania walikuwa wamejiandaa kwa pambano hilo, baadhi wakiwa wamepata hasara yakutumia nauli kutoka mikoani ili kuja kupata burudani hiyo," alisema Mopao.

Mwakinyo alitarajiwa kupanda ulingoni kupigana na mpinzani wake Julius Indongo kutoka Namibia, lakini mapema siku ya pambano hilo, alieleza hatapanda ulingoni kwa kile alichodai kukiukwa kwa vipengele vya mkataba waliokubaliana na waandaaji wa pambano hilo, Paf Sports Promotion.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LEWANDOWSKI AWINDWA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Poland, Robert Lewandowski, 35, anawindwa na miamba ya Ligi Kuu ya Saudi Arabia. ***(Sport)***

### NETO AFUATILIWA ARSENAL

ARSENAL itaendelea kumfuatilia mshambuliaji wa Wolves na Ureno, Pedro Neto, 23, kwa matumaini ya kumsajili mchezaji huyo katika uhamisho wa Januari. ***(Mirror)***

### DIOMANDE NAYE ATAKIWA

ARSENAL pia inamfuatilia mchezaji wa Sporting Lisbon na mlinzi wa Ivory Coast, Ousmane Diomande, 19. ***(Givemesport)***

### CHELSEA NA VLAHOVIC

MKURUGENZI wa Michezo wa Juventus, Cristiano Giuntoli, amesema Chelsea ilishindwa kumsajili mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic, 23, kwa sababu hawakutoa ofa ambayo ilikidhi thamani iliyotakiwa na klabu hiyo ya Italia. ***(La Repubblica, kupitia Goal)***

### LINGARD HAYUKO SAWA

KLABU ya West Ham iliamua kutomsajili mshambuliaji wa England, Jesse Lingard, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Nottingham Forest, kwa sababu hayuko sawa. ***(Football Insider)***

### GIMENEZ ATAJWA CHELSEA

ARSENAL, Chelsea na Tottenham Hotspur zimeonesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa Feyenoord na Mexico, Santiago Gimenez, 22. ***(Fijaches)***

### WAAMUZI WASAKWA SAUDIA

SHIRIKISHO la Soka la Saudi Arabia, limewatafuta waamuzi wakuu wa Ligi Kuu England, akiwamo Michael Oliver kuhusu kuchezesha Ligi ya Saudia. ***(Telegraph)***

### MALEN KUMRITHI SALAH

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, ana nia ya kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Donyell Malen mwenye umri wa miaka 24, kutoka Borussia Dortmund huku akitafuta mchezaji wa kumsaidia winga wa Misri, Mohamed Salah, 31. ***(Bild, via Express)***

### BOATENG KURUDI BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inajadiliana kuhusu uwezekano wa kumsajili tena beki wa zamani wa Ujerumani, Jerome Boateng mwenye umri wa miaka 35, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Lyon mwishoni mwa msimu uliopita. ***(Sky Sports)***

### BRANTHWAITE MKATABA MPYA

EVERTON iko tayari kumpa mlinzi wa England chini ya umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite mkataba mpya. ***(Football Insider)***

### MARTINEZ MIEZI MIWILI NJE

BEKI wa Manchester United, Lisandro Martinez, 25, atakuwa nje ya uwanja kwa muda wa miezi mitatu kutokana na jeraha la mguu. Mlinzi wa kimataifa wa Argentina 25, alikosa mwisho wa msimu uliopita baada ya kupata jeraha kwenye mfupa wa unyayo wa mguu Aprili. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG AFUNGUKA SABABU KUZOMEWA

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amesema "naelewa" zomea ya mashabiki baada ya Manchester United kufungwa bao 1-0 na Crystal Palace, Jumamosi.

**Kikosi cha Roy Hodgson kilipeleka kichapo cha tano msimu huu kwa United, jambo lililosababisha hisia mbaya kutoka kwa mashabiki wa nyumbani.**

"Naelewa," alisema Ten Hag kocha Man United baada ya mchezo huo wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Tunapocheza nyumbani au ugenini na tunacheza na Crystal Palace, lazima tushinde, kwa heshima zote, najua kila mchezo kwenye Ligi Kuu ni mgumu sana, lazima ucheze kwa uwezo wako wote na ninaelewa mashabiki wanatarajia ushindi na sisi hatukushinda, tulishindwa."

**Tunapaswa kuwa thabiti zaidi, mahitaji ni sisi kupata ushindi mfululizo na...**

Ni mara ya kwanza tangu mwaka 1989 kwa Man United kupoteza mechi nne kati ya saba za kwanza za ligi.

Na inaiacha timu hiyo ya Ten Hag ikiwa nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu na Mholanzi huyo alisema kunaweza kuwa na "visingizio" kwa kuanza vibaya kwa msimu.

"Tunapaswa kuwa thabiti zaidi," aliongeza Ten Hag.

"Mahitaji ni sisi kupata ushindi mfululizo na tunapaswa kufanya vizuri zaidi kuliko sasa. Naweza kukupa sababu, lakini utaeleza kama kisingizio na hakuna visingizio, tunahitaji kushinda."

Wakati huo huo, kocha wa Palace, Roy Hodgson mwenye umri wa miaka 76, aliachwa kusherehekea kuendeleza mbio zake za kutopoteza kwenye Uwanja wa Old Trafford kufikia mechi tano; nne akiwa na Palace na moja na Watford.

"Nimefurahishwa na rekodi hii, lakini ninachofurahia zaidi ni jinsi timu ilivyocheza na kuwafurahisha wachezaji," alisema Hodgson, ambaye timu yake ilipoteza 3-0 nyumbani dhidi ya Man United kwenye Kombe la Carabao Jumanne.

"Si rahisi kuja hapa kwa mara ya pili katika siku chache na kupata matokeo bora zaidi."

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 728,

MECHI KALI

FULHAM
VERSUS
CHELSEA

1 | 3.71
X | 3.50
2 | 2.02

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ARTETA AMSIFIA HAVERTZ KWA BAO LA KWANZA

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alijivunia wachezaji wake baada ya Kai Havertz kufunga kwa mkwaju wa penalti na kuisaidia Arsenal kushinda mabao 4-0 dhidi ya Bournemouth, juzi kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Kiungo huyo wa kati wa Ujerumani alifunga penalti hiyo na kumfanya afunge bao lake la kwanza klabu hiyo tangu ajiunge nayo kipindi cha majira ya joto.

Baada ya ushindi huo, Arteta alizungumza juu ya furaha aliyokuwa nayo kwa upande wake kutokana na kumpa Havertz fursa ya kupata bao.

Alisema: "Kwa kweli nimefurahi kwa ushindi huo, lakini ninafurahi zaidi kuwa sehemu ya kitu, sehemu ya timu inayoonesha sifa za kibinadamu ambazo wameonesha leo.

"Wamefanya kwa njia ya asili, nimefurahi wamefanya uamuzi huo, ninawashukuru sana mashabiki wetu jinsi walivyoimba jina lake, wamemfanya ajisikie kama anavyojisikia leo na kama kuna mtu katika chumba cha kubadilishia nguo anayestahili hivyo, ni Kai Havertz. Nina furaha sana kwake."

Ushindi huo unaifanya Arsenal kupitwa pointi moja na vinara wa ligi hiyo, Manchester City ambayo ilichapwa mabao 2-1 na Wolves.

Arteta anaamini kuwa bao hilo litakuwa msaada mkubwa kwa Havertz kwani 'Washikabunduki' hao wanatazamia kupata zaidi kutoka kwa mchezaji huyo.

Alisema: "Labda itabadilisha kila kitu, lakini kwanza kabisa ikiwa alikuwa na alama za swali juu ya jinsi tunavyohisi juu yake, jinsi tunavyompenda, ni kiasi gani tunathamini kila kitu anachofanya.



# Martinez aweka historia Serie

**MILAN,** Italia

LAUTARO Martinez aliweka historia kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa kufunga manne akitokea benchi na kuwawezesha Inter Milan kushinda 4-0 dhidi ya Salernitana Jumamosi na kuwarudisha kileleni mwa msimamo.

Fowadi huyo wa Argentina ndiye mchezaji wa kwanza kufunga mabao manne akitokea benchi katika misimu 30 iliyopita kwenye Serie A, tangu msimu wa 1994-95.

Wenyeji walikuwa wameikazia Inter kipindi cha kwanza, lakini walisambaratishwa baada ya Martinez kuingia uwanjani dakika tisa baada ya kipindi cha mapumziko na kufunga mabao manne ndani ya dakika 27, likiwamo moja la mkwaju wa penalti.

Inter walikuwa wameshuka kwa pointi tatu chini ya AC Milan kwenye msimamo baada ya wapinzani wao kushinda 2-0 dhidi ya Lazio mapema Jumamosi, lakini walirejea kileleni wakiwa na pointi 18 kutokana na mechi saba. Salernitana wapo nafasi ya 19 wakiwa na pointi tatu.

Nahodha wa Inter, Martinez sasa amefunga mabao tisa katika mechi saba za Serie A na anaongoza kwa kuwa mfungaji bora wa ligi.

"Nilifunga mabao ma
lakini jambo la mu
ni kwamba Inter ilis
mchezo," alisema akiia
Sky Sport Italia, na kuo
kuwa kubadilisha m
baada ya kupoteza 2-1 dh
Sassuolo Jumatano kuli
kipaumbele.

"Ilikuwa muhimu k
Tulipoteza mchezo huk
Siro ambao tuliruhusu m
mawili kutokana na m
yetu, kwa hiyo tulilaz
kushinda leo (juzi)."

Huku Inter wakit
hatua za mwanzo za m
Salernitana alipata nafas
na kufanikiwa kudhibit
katika kipindi cha kwan

# 573,060

# JACKPOT
Lorem ipsum
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/10/23 | 22:00 | Newcastle vs Paris St Germain | 2.39 | 3.52 | 2.58 |
| 02. 04/10/23 | 22:00 | Celtic vs Lazio | 2.73 | 3.43 | 2.31 |
| 03. 04/10/23 | 22:00 | Borussia Dortmund vs AC Milan | 2.30 | 3.47 | 2.73 |
| 04. 04/10/23 | 22:30 | Burgos vs Leganes | 2.37 | 2.97 | 3.02 |
| 05. 04/10/23 | 22:30 | Sporting Gijon vs Elche | 2.53 | 3.12 | 2.68 |
| 06. 05/10/23 | 16:00 | Mtibwa Sugar vs Singida BS FC | 2.48 | 2.94 | 2.89 |
| 07. 05/10/23 | 19:45 | Marseille vs Brighton | 2.80 | 3.55 | 2.27 |
| 08. 05/10/23 | 19:45 | SC Freiburg vs West Ham | 2.49 | 3.43 | 2.58 |
| 09. 05/10/23 | 19:45 | Sporting Lisbon vs Atalanta | 2.22 | 3.36 | 3.01 |
| 10. 05/10/23 | 19:45 | Rakow Czestochowa vs Sturm Graz | 2.37 | 3.25 | 2.85 |
| 11. 05/10/23 | 22:00 | BK Hacken vs Karabakh | 2.47 | 3.35 | 2.65 |
| 12. 05/10/23 | 22:00 | Maccabi Haifa vs Panathinaikos | 2.25 | 3.36 | 2.96 |
| 13. 05/10/23 | 22:00 | PAOK vs Eintracht Frankfurt | 2.70 | 3.36 | 2.55 |

## MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 02/10/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 1059 | Rodina Moscow vs KamAZ | 1.62 | 3.58 | 4.64 |
| 16:00 | 1131 | FK Mladost Gat vs GFK Dubocica | 1.71 | 3.33 | 4.43 |
| 16:00 | 2265 | Asyut Petroleum vs Proxy SC | 1.90 | 3.31 | 3.67 |
| 16:00 | 4937 | Aswan vs Nogoom EL Mostakbal | 1.86 | 3.16 | 4.08 |
| 16:00 | 5680 | Misr Lel Makasa vs El Sekka El Hadid | 3.00 | 3.20 | 2.20 |
| 16:30 | 1403 | Akron Tolyatti vs FK Khimki | 1.97 | 3.13 | 3.53 |
| 17:00 | 5142 | SC Dnipro 1 vs FC Metalist 1925 | 1.42 | 4.04 | 6.26 |
| 17:30 | 3238 | Sanat Mes Kerman FC vs Fajr Sepasi | 1.85 | 3.05 | 4.00 |
| 18:00 | 1984 | FC Politehnica Iasi vs Petrolul Ploiesti | 2.39 | 3.08 | 2.88 |
| 18:00 | 2468 | Mosaset AL Bireh vs Hilal Al-Quds | 6.05 | 4.23 | 1.41 |
| 18:00 | 4124 | Pars Jonoubi Jam vs Mes Shahr-e Babak | 2.04 | 2.70 | 4.17 |
| 18:00 | 4672 | Atromitos vs Asteras Tripolis | 2.13 | 3.06 | 3.58 |
| 18:10 | 1856 | Al Qadisiyah vs Al Jabalain | 1.55 | 3.55 | 5.47 |
| 18:10 | 4101 | AL Qaisoma vs Al Orubah | 3.08 | 3.13 | 2.15 |
| 18:30 | 1321 | Sigma Olomouc B vs Dukla Prague | 2.93 | 3.39 | 2.11 |
| 19:00 | 1018 | Hapoel Ramat Gan vs Hapoel Acre | 2.48 | 3.21 | 2.74 |
| 19:00 | 1689 | AEZ Zakakiou vs Pafos FC | 7.25 | 4.87 | 1.36 |
| 19:00 | 1773 | Zeljeznicar vs Siroki Brijeg | 1.64 | 3.71 | 4.57 |
| 19:00 | 1998 | Istra vs Lokomotiva Zagreb | 2.36 | 3.13 | 2.73 |
| 19:00 | 2076 | Hapoel Afula vs Ironi Tiberias | 3.31 | 3.47 | 2.04 |
| 19:00 | 2431 | Maccabi Jaffa vs SC Kfar Qasem | 2.09 | 3.32 | 3.32 |
| 19:00 | 4301 | Sokol Saratov vs FC Alania Vladikavkaz | 3.83 | 3.33 | 1.82 |
| 19:00 | 4305 | Din. Tirana vs Vllaznia | 3.90 | 3.30 | 1.79 |
| 19:00 | 4978 | Apoel Nicosia vs Ethnikos Achnas | 1.32 | 4.87 | 8.70 |
| 19:30 | 1732 | Torino vs Verona | 1.84 | 3.45 | 4.64 |
| 19:30 | 2819 | Sassuolo vs Monza | 2.24 | 3.75 | 2.98 |
| 19:30 | 5188 | Chateauroux vs Red Star | 3.14 | 3.09 | 2.26 |
| 20:00 | 1011 | Penafiel vs Nacional Madeira | 2.07 | 3.27 | 3.27 |
| 20:00 | 1415 | Kayserispor vs Basaksehir | 2.58 | 3.25 | 2.56 |
| 20:00 | 1618 | Goeztepe vs Adanaspor | 1.62 | 3.48 | 4.84 |
| 20:00 | 2051 | IK Brage vs Skovde Aik | 1.69 | 3.77 | 4.71 |
| 20:00 | 2930 | OFI Crete vs AEK Athens | 6.66 | 3.75 | 1.52 |
| 20:00 | 3584 | Odense vs Lyngby | 2.25 | 3.35 | 3.00 |
| 20:00 | 4357 | Jonkopings Sodra vs Ostersunds | 2.68 | 3.31 | 2.54 |
| 20:00 | 4856 | Gornik Zabrze vs Zaglebie Lubin | 2.47 | 3.24 | 2.53 |
| 20:00 | 5263 | AL Najma vs AL Arabi (SA) | 3.70 | 3.15 | 1.88 |
| 20:00 | 5640 | Elfsborg vs Varbergs Bois | 1.14 | 6.48 | 12.16 |
| 20:00 | 5807 | Utsiktens BK vs AFC Eskilstuna | 1.82 | 3.61 | 4.09 |
| 20:10 | 2259 | Malmo vs Brommapojkarna | 1.26 | 5.25 | 7.87 |
| 20:30 | 3783 | Beitar Jerusalem vs Hapoel Tel Aviv | 2.21 | 3.38 | 2.77 |
| 21:00 | 4152 | Maastricht vs FC Eindhoven | 2.38 | 3.36 | 2.65 |
| 21:00 | 4929 | Jong Utrecht vs NAC Breda | 3.52 | 3.62 | 1.87 |
| 21:10 | 2137 | HNK Sibenik vs NK Dugopolje | 1.56 | 3.78 | 4.84 |
| 21:45 | 1702 | Fiorentina vs Cagliari | 1.49 | 4.42 | 6.57 |
| 21:45 | 1730 | AC Ajaccio vs Bastia | 2.23 | 2.97 | 3.27 |
| 22:00 | 1081 | Fulham vs Chelsea | 3.71 | 3.50 | 2.02 |
| 22:00 | 1265 | Espanyol vs Racing Ferrol | 1.56 | 3.81 | 5.34 |
| 22:00 | 5215 | Las Palmas UD vs Celta Vigo | 2.63 | 3.15 | 2.84 |
| 22:15 | 5144 | SCU Torreense vs CF Os Belenenses | 1.72 | 3.42 | 4.49 |
| 22:15 | 5613 | Gil Vicente vs Casa Pia Atletico | 2.30 | 3.18 | 2.98 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# TAMTHILIA YA CHANDA KUANZA RASMI LEO MAISHA MAGIC BONGO

**Na Mwandishi Wetu**

TAMTHILIA mpya ya Chanda iliyosheheni waigizaji maarufu na wenye mvuto kama vile Mwijaku, Feza Kessy, Hidaya Njaidi na wengineo wengi itaanza kurushwa rasmi leo, Jumatatu kuanzia saa 1:30 kupitia DStv ndani ya Chaneli ya Maisha Magic Bongo namba 160, imeelezwa.

**Waigizaji hao maarufu na wenye mvuto wataonesha umwamba wao wa kuigiza hasa ikizingatiwa hadithi inayobebwa na tamthilia hiyo imejaa vituko, visa, mikasa, vitimbi na mikikimikiki kibao na itakuwa ikirushwa kila Jumatatu hadi Jumatano saa 1:30 usiku.**

Msimu wa kwanza wa Chanda unaelezea maisha magumu ya Yaz Diwani, (Christopher Moris) na Azra Shakombo (Fezza Kessy). Huku akiwa amezaliwa katika familia tajiri na iliyotukuka, Yaz, mrithi pekee wa himaya ya Diwani, anajikuta katika kimbunga cha penzi zito na Azra, binti wa mpishi na rafiki mwaminifu wa baba yake, Hamza Shakombo (Jafary Makatu).

Akizungumzia tamthilia hiyo, Mtayarishaji Isike Samwel, alisema: "Tunafuraha kubwa kuwaletea Watanzania tamthilia ya Chanda. Hii si tu tamthilia ya kawaida, ni mfano wa vipaji maridhawa tulivyo navyo. Waigizaji wetu ni bora zaidi na tunaamini tamthilia ya Chanda itaweka alama katika tasnia hii kwa kuwaburudani bora kuwahi kutokea.

Akielezea kwa nini watazamaji waingalie Chanda, alisema alianza kutaja kuwa kuna fundisho kubwa katika migongano na changamoto za kifamilia kupitia maisha ya familia ya Diwani na Shakombo ambapo itashuhudiwa mapambano ya madaraka, vifungo vya urafiki, na uzito wa urithi huku familia mbili zikiingiliana katika safari ya upendo, siri, na uaminifu.

Pia alitaja hatima ya mapenzi ya siri kwamba ni kiini cha Chanda na kwamba ni mapenzi kati ya Yaz na Azra kutoka harusi ya kifahari ya uswahilini hadi changamoto wanazokabiliana nazo, ambayo ni safari iliyojaa shauku, siri na uaminifu usioyumba.

Aidha, alisema ina wahusika wa kike wenye nguvu na uthabiti wa wahusika kama Dida Diwani, ambaye anawajibika katika jukumu lake kwa uthabiti, matamanio na mguso wa hila na Azra anayeonyesha uthabiti na uaminifu anapokabiliwa na dhiki pamoja na mambo kibao ya kuvutia.

Meneja Masoko upande Maudhui kutoka MultiChoice Tanzania, Noel Mulumba, alisema: "Wakati wote tunazingatia sana maoni ya watazamaji wetu na yote hii tunafanya ili kuhakikisha kuwa mtazamaji wetu anapata kile anachopenda."

Pia alibainisha kuwa DStv kupitia Maisha Magic Bongo imedhamiria kuleta mabadiliko chanya katika tasnia ya filamu hapa nchini na barani Afrika kwa ujumla.

Naye Ofisa Maendeleo ya Filamu kutoka Bodi ya Filamu Tanzania, Ally Makata, alisema serikali kupitia Bodi ya Filamu imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimba ikiwamo DStv katika kuhakikisha inapeleka mbele gurudumu la maendeleo ya filamu hapa nchini.



Meneja Masoko wa Maudhui wa MultiChoice Tanzania, Noel Mulumba, katika uzinduzi wa Tamthilia ya Chanda, itakayorushwa na DStv ndani ya Chaneli ya Maisha Magic Bongo kuanzia leo Jumatatu. Tukio hilo lilifanyika Dar es Salaam wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

# Mzize awataja Mayele, Gamondi

INATOKA UK. 24

kwa ajili ya kupachika bao jambo ambalo alilitekeleza kwa vitendo dakika ya 66, akifunga kwa kichwa.

Nyota huyo alianzia benchi akichukuwa nafasi ya Musonda na kufanikiwa kufunga bao hilo baada ya kuunganisha mpira wa krosi iliyopigwa na Joyce Lomalisa.

"Kocha aliniambia niwe makini na kutofanya makosa kwenye eneo la hatari na kutumia vizuri mipira ya krosi na nilifanikiwa kuipeleka timu hatua ya makundi.

Kuhusu kushangilia staili ya kutetema ambayo alikuwa akiitumia Mayele, alisema bado anaishi moyoni mwake na kwamba alikuwa mtu kumtia moyo.

# Simba hii imeenda

INATOKA UKURASA 24

Baleke, Kibu na Mzamiru Yassin akiwaingiza Bocco, Willy Onana na Sadio Kanoute ambaye waliuchangamsha mpira na timu ikaanza kutembea.

Hata hivyo, wachezaji wa Simba walionekana kucheza kwa tahadhari kubwa hasa baada ya kupata bao, wakionekana kutaka matokeo hayo yasalie kwani wangeweza kuwavusha kwenye hatua ya makundi na ilikuwa hivyo, huku wachezaji wa Power Dynamos wakionekana kuchoka kadri muda ulivyozidi kusonga mbele kwa sababu ya kucheza kwa kasi na kutumia nguvu hasa kipindi cha kwanza na cha pili mwanzoni.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 2, 2023

Nipashe




Ten Hag afunguka kuzomewa UKURASA 21

HAMNIWEZI...



Beki wa kulia wa Simba, Shomari Kapombe, akiwatoka wachezaji wa Power Dyanamos katika mchezo wa mkondo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Afrika kuwania kufuzu hatua ya makundi uliopigwa Azam Complex, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa sare ya 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba hii imeenda

## ●●● Yatinga makundi ilipozoea Ligi ya Mabingwa, Bocco adhihirisha ukongwe wake, Dynamos ikifurushwa...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya nne ndani ya miaka sita, Klabu ya Simba imefanikiwa kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya jana kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Power Dynamos ya Zambia kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

**Simba imefanikiwa kusonga mbele kwa mabao yake mawili ya ugenini kwani ililazimisha timu hiyo kutoka sare ya mabao 2-2 kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa, Ndola nchini Zambia, Septemba 16, mwaka huu.**

Kwa matokeo ya jumla ni kwamba timu hizo zimefunga mabao 3-3, lakini wawakilishi hao wa Tanzania wananufaika kwa kufunga mabao mengi ugenini.

Hata hivyo, haikuwa rahisi kwani walilazimika kusubiri hadi dakika ya 68 kuweza kusawazisha bao walilotanguliwa.

Zilikuwa ni juhudi za mtokea benchini nahodha John Bocco, akiwa wingi ya kulia alipiga krosi ambayo ilisukumizwa wavuni na beki wa kulia wa Power Dyanamos, Kondwani Chiboni, katika harakati za kukata kuuokoa.

Matokeo hayo pia yameweka rekodi kwa timu mbili za Tanzania kwa mara ya kwanza katika historia ya michuano hiyo kutinga zote kwa pamoja hatua ya makundi.

Wakati Yanga ikitinga mara ya pili hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika juzi kwenye historia ya timu hiyo, mwaka 1998 na mwaka huu, Simba imetinga kwa mara ya tano, kwanza ikiwa ni 2003 ilipoitoa Zamalek ya Misri.

Imeshawahi kufanya hivyo pia 2018 ilipoifunga Nkana Red Devils jumla ya mabao 4-3, ikifungwa mabao 2-1 nchini Zambia na kushinda 3-1 Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikitinga tena mwaka 2021 ilipoichakaza FC Platinum ya Zimbabwe mabao 4-1, ilifungwa bao 1-0 ugenini na kushinda 4-0 nyumbani, na mwaka jana iliingia kwa kuiadabisha Primeiro de Agosto ya Angola kwa jumla ya mabao 4-1, ikishinda ugenini 3-1, kabla ya kushinda nyumbani bao 1-0.

Wageni Power Dynamos walianza mechi kwa kasi ikionekana kabisa kuhitaji bao la haraka na walifanya hivyo kwa kulishambulia lango la Simba kwa kipindi cha dakika tano mfululizo.

Dakika ya sita ndipo Simba ilipofanya shambulizi la kwanza kwenye lango la Power Dynamos, Kibu Denis akiwa pembeni kidogo ya lango, alimpenyezea Jean Baleke, lakini alichelewa kupiga kabla ya mabeki kuokoa.

Safari ya Simba kwenda kwenye makundi ilitiwa doa dakika ya 16 ya mchezo pale straika Andy Boyeli alipopachika bao kwa shuti kali nje ya eneo la hatari. Yalikuwa ni makosa ya wachezaji wa Simba ambao licha ya wachezaji sita kuwa karibu naye, lakini wote walionekana kukabia macho, na kumruhusu kuutengeneza mpira vizuri na kuvuta hatua kadhaa kabla ya kuachia mkwaju uliopita kulia kwa kipa Ayoub Lakred na kujaa wavuni.

Bao hilo lilionekana kuwashtua mashabiki wa Simba waliokuwa uwanjani na wachezaji wao kwani hakukuwa na utulivu kiasi cha kuwapa nafasi Power Dynamos kupumzika kwa kurudi nyuma na kulinda walichokipata.

Baleke kama angetulia angeweza kusawazisha bao dakika ya 34, lakini kukosa utulivu na kuzongwa na mabeki wa Power Dynamos alipiga shuti dhaifu ikawa mboga kwa kipa Willard Mwanza.

Dakika moja baadaye, Baleke tena aliupata mpira akiwa pembeni kidogo ya lango alikung'uta shuti lililopanguliwa na kipa Mwanza, kabla ya kugonga nguzo ya pembeni na kuwa kona.

Saido Ntibazonkiza naye alijaribu mkwaju mkali uliopaa juu.

Kipindi cha pili Kocha Mkuu Robertinho Oliveira alifanya mabadiliko kwa kuwatoa

INAENDELEA UKURASA 23

## Mzize awataja Mayele, Gamondi bao Al-Merrikh

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Klabu ya Yanga, Clement Mzize, ametoa siri ya bao pekee alilofunga dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan kwenye mechi ya mkondo wa pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika akiwataja, Fiston Mayele na Miguel Gamondi kuhusika.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi na Yanga kushinda 1-0, hivyo kufuzu hatua ya makundi kwa mara ya kwanza baada ya miaka 25, Mzize alitokea benchi akichukua nafasi ya Kennedy Musonda.

Akizungumza na Nipashe baada ya mchezo huo, Mzize alisema anamshukuru aliyekuwa mchezaji wa timu hiyo, Mayele kwani ushauri wake unampa mafanikio ambayo hakuwahi kuyatarajia.

Alisema siku zote kabla ya Mayele kuondoka Yanga na kwenda kujiunga na Pyramids ya Misri, alikuwa akimshauri vitu vingi kimchezo kutokana na uwezo aliokuwa nao.

"Ninamshukuru Mayele, ushauri wake umenisaidia kwa kiasi kikubwa, ni mtu ambaye amenifanya niwe na historia kwenye maisha ya mpira," alisema Mzize.

Aidha, alishukuru kufunga magoli mawili katika michuano ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika dhidi ya Al-Merrikh ugenini na nyumbani.

Katika mchezo wa kwanza uliopigwa Rwanda kutokana na Sudan kuwa katika machafuko ya kisiasa, Yanga ilishinda mabao 2-0, yakifungwa na Musonda na Mzize, hivyo kufuzu hatua ya makundi kwa jumla ya mabao 3, kuhusu Gamondi, alisema alimtaka kutumia vizuri mipira ya krosi

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >